

# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

UPEPO WA MABADILIKO WA KIBIASHARA



# TRADE WARS

JE, UKO TAYARI KUSHIRIKI  
PASAKA?

SIKU YA KUANGALIWA NA  
SIKUKUU ZA MIKATE  
ISIYOTIWA CHACHU

## Unabii wa Habari za Biblia

Katika nakala hii:

**2. Kutoka kwa Mhariri:Upepo wa Mabadiliko ya Kibiashara** Kulingana na kura ya kujiondoa kwa Waingereza,hatua zingine za Rais wa Marekani Donald Trump,mipango ya Waingereza,na matarajio ya Wachina,biashara ya kimataifa inabadilika.Je! Hii inaweza kusababisha vita vya kibiashara na baadaye vita halisi?

**7. Je!Uko tayari kuila Pasaka?** Pasaka ni baada ya jioni ya Machi 29 mwaka huu.Je! Utakuwa tayari kuila Pasaka?

**13. Usiku wa Kuzingatiwa na Siku za Mkate Usiotiwa Chachu** Hii inakuja baada ya Pasaka.Je! Unajua zaidi kuhusu siku hizi?

**21. Jisomee Kozi ya Biblia Jaribio la 3** Hili ni jaribio linalojumuisha somo la 9-12 ya Kozi ya Biblia.

**34. Ufalme wa Mungu na Shabaha za Umoja wa Mataifa** Je! Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya 2030 na mkataba wa Pari italeta mazingira safi na ustawi wa kiuchumi?Ama ni habari ya uongo?

**Jalada la Nyuma:**Intaneti na Redio Hii inaonyesha mahili watu wanaweza kupata ujumbe kutoka kwa Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG).

**Kuhusu Jalada la Mbele:**Biashara ya kimataifa inabadilika.Je! Hii yaweza kuleta vita vya kibiashara na baadaye vita halisi? Muundo wa jalada na Debra Castro,Vitabu vya Mnazareti.

**Unabii wa Habari za Biblia** inachapishwa na Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG),1036 W.Grande Avenue,Grover Beach,CA,93433.<http://www.ccog.org>

©2018 Kanisa la Mungu Linaloendelea.Imechapishwa Marekani.Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi.Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi,kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu.Endapo haungependa kuupokea gazeti hili,wasiliana na afisi yetu ya Grover Beach.Maandiko yamenukuriwa toka New King James Version © Thomas Nelson,Inc,Publishers,used

by permission isipokuwa pale tu tumeelezwa vinginevyo.

**Unabii wa Habari za Biblia**  
**HUWEZESWA KWA MICHANGO**  
**YENU.**

**Mhariri Mkuu:**Bob Thiel

**Nakala/Mhariri Msaidizi:**Joyce Thiel

**Masahihisho:**John Hickey;SBC Course Assister;Shirley Gestro.

**Picha:**Picha zote zimetokana na familia ya Thiel na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa ni chanzo hakikutajwa;itakuwa ni kwa sababu inamaanika kwamba chanzo husika kiliachia picha iwe matumizi ya umma pasipo masharti yoyote).



KUTOKA KWA MHARIRI MKUU:BOB THIEL

### Upopo wa Mabadiliko wa Kibashara

Kanisa la Mungu limeonya kuhusu masuala ya kibashara kwa miongo mingi.Na kwa miaka iliyopita,tumeona maendeleo mengi ambayo yanafungamana na yale tumeyasema ambayo Biblia inatabiri.

Hapo mnamo mwaka wa 1971, Mchungaji Mkuu wa Kanisa la awali ya Mungu Ulimwenguni Kote hati Herbert W.Armstrong aliandika yafuatayo:

#### Vita Vya Kibashara Vinajitokeza ili Vichokore Vita vya Ulimwengu wa III?

Twaweza kuweka kizuizi dhidi ya nchi zingine kwa kupandisha ushuru,kuanzisha VITA VYA KIBIASHARA ambapo kwa wakati mmoja itachokora vita vya nyuklia ambavyo VITATUHARIBU-ama,wafanyakazi wa Marekani lazima WAFIKIE kiwango cha wafanyakazi wengine katika nchi zingine,kwa kupunguza viwango vya kuishi.Ni dhahiri kwamba Wafanyakazi wa Marekani hawatakulali kupunguza viwango vya kuishi.Na ikiwa hawataweza-basi,MWANDIKO UKO UKUTANI MWA TAIFA LETU.(Armstrong HW.Trade War Looming to Trigger World War III? Plain Truth, March 1971)

Na wakati wazo lake la kimsingi la wakati lilipita,ni ukweli kwamba masuala ya biashara yatakuwa sababu ambayo itachokora vita vya tatu vya dunia.Vita ambavyo vitakuwa dhidi ya Marekani,Canada,na Ulaya na nguvu

itakayojipanga (Ufunuo 17:12-13).Ulaya ambao wamekasirika na Uingereza kwa kujiondoa kwa Umoja wa Ulaya na ambao pia wamekasirika na Marekani kwa sababu ya mambo mengi (pamoja na maamuzi ya Rais wake Donald Trump na bunge lake).

Miongo mingi iliyopita, Gene Hogberg wa Kanisa la awali ya Mungu la Ulimwenguni Kote aliandika yafuatayo:

ANGALIA hatima ya Ulaya ya Magharibi. ...

Ulaya mpya wa Magharibi ambayo pengine inatawala nusu ya biashara yote ya ulimwengu,kwa mipango maalum na mataifa mengi ambayo yanazalisha mali ghafi.

“Umoja wa Mataifa ya Ulaya” ambao wana sarafu moja-sarafu ambayo itakuwa na nguvu na itachukua nafasi ya dola ya Marekani na itatumika kama sarafu ya biashara ya ulimwengu.Ulaya ilio na umoja itaendelea kuwa na nguvu ya kijeshi ili walinde kiwango cha maisha yao ya kipekee na nafasi yao ya kwanza katika ulimwengu.Hayo ni maono mazuri?

La hasha.

Nguvu kama hiyo ya Ulaya iko karibu na upeo. ...

#### Kikwazo Kikubwa

Kikwazo kikubwa kinachozua kufanikisha juhudini zima bado kipo.Ni suala la ubishi wa kisiasa. ...

Ikiwa Uingereza haikufurahishwa na “jinsi mambo yanavyoenda katika Soko la Kawaida mnamo mwisho wa 1975,basi Uingereza

pamoja na nchi ambayo haikufurahishwa ,wanaweza kujiondoa.Kwa hivyo Uingereza watajiondoa-watatoka kwa Ulaya...

Ni dhahiri kwamba Ulaya inayopanuka haitavumilia ukosefu wa uwajibikaji wa kifedha ambao Marekani wanao-ama kuangalia njia nyingine ikiwa Marekani wataweka taasisi ya kisheria ya kuhifadhi biashara.Jinsi mambo yanavyoendelea,ni muda kitambo kabla Ulaya wajiondoe kutoka kwa sarafu ya dola.Tayari wameweka mitambo yaendelee kufanya kazi. ...Ikiwa dola itaanguka,sarafu mpya ya Ulaya itafanya kazi kama sarafu yenye nguvu ya kufanya biashara ulimwenguni.Dola itakuwa bidhaa isiyo na thamani.Mataifa yanayofanya biashara ulimwenguni yatafanya biashara na sarafu hii ya "mnyama" ili wapate kudumu.(Hogberg G.Rising World Colossus.Plain Truth,May 1971).

#### **Ujiandae kwa Vita vya Kibiashara**

Ulimwengu huru ya miaka 40 ya ustawi usio wa kawaida utakuja kukoma.Usaidizi kutoka Marekani-taifa la magharibi linaloongoza katika biashara-ili kusaidia kudumisha biashara huru linabomaka haraka.

Badala yake, wanaduta katika kuta za Kongamano linalotoa maonyo kwa washirika wa biashara wafungue soko ama wakabiliane na kisasi cha kulipa ushuru ya juu...

Bw.Reagan kwa huzuni yuafahamu mahali ulinzi huu usio na mwelekeo unaenda.Awali alipokuwa akikana ombi la mlinzi kutoka kwa kiwanda fulani,Rais aliamsha kumbukumbu la huzuni-awamu ya sheria ya ushuru wa Smoot-Hawley. "Wengine wetu twakumbuka mwaka wa 1930,wakati muswada wa biashara uliokuwa hatari sana katika historia,ya sheria ya ushuru wa Smoot-Hawley ulisaidia kuangusha taifa hili na ulimwengu katika miongo ya huzuni na ukosefu wa tumaini," alimwambia waskilizaji wa radio.

"Kuanzia leo,ikiwa pepo ya Smoot-Hawley itaweka kichwa chake kibaya katika Kongamano,ikiwa Kongamano litaweka huzuni-kwa kufanya muswada,nitaipiga vita."

#### **Alichofanya Smoot-Hawley**

Je! Ni jinsi gani muswada wa Smoot-Hawley ulileta uharibifu? Wajibu wake mkubwa katika kuleta Huzuni Kubwa ulielezwa katika nakala ya Septemba 5 ya Jarida la Ukuta wa Mtaa,katika makala ilioandikwa na wahariri wake,Robert L.Bartley. "Kuanguka kwa soko la hisani la 1929 kulikuja katikati ya mdahalo katika Kongamano juu ya ushuru," aliandika Bw.Bartley. "Imezidi kuongeza bidhaa baada ya bidhaa kwa orodha ya ulinzi.Kati ya 1930,muswada wa Smoot-Hawley ulifanywa kuwa sheria,na ushuru ya juu sana katika historia ya ulimwengu." "Kile ambacho kingekuwa marekebisho ya kawaida",alioneza Bw.Bartley," kikageuka kuwa Huzuni Kubwa." ...wakati akaunti za kimataifa zilifungwa,na uchumi wa ulimwengu ukakabwa roho." ...

#### **Mabadiliko hatari za Usalama**

Wataalam wengine wanaonya kwamba viongozi wa kisiasa wa Marekani-wanaoitikia wito wa kuwa na nafuu wa mashindano kutoka kwa majimbo yao-wanaweza puuzia walilokumbana nalo la Huzuni Kubwa:Kwamba upungufu mbaya wa biashara ya ulimwengu uliongeza nguvu kwa kuongezeka kwa ubeberu katika Asia na Ulaya,hasa Japani na Ujerumani.

Tangia mwaka wa 1945 Japani wamechagua ufanyi biashara kama njia ya kupata mamlaka,heshma na ukombozi.Ujerumani,hasa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani,inategemea sana biashara ya ulimwengu,wakiiza nje

theluthi moja ya bidhaa wanazozitengeneza.

Upatikanaji wa soko la Marekani ni muhimu kwa uchumi wa Japani na mataifa mengine ya Kilindi cha Pasifikasi,aliandika mhariri wa kimataifa John McLaughlin, "na pengine kwa uimara wao."Ikiwa ulinzi utaendelea,ni nini itafanyikia Japani na Ulaya wa magharibi,ambao moyo wao wa uchumi uko Ujerumani? Ulinzi,unaoelekea kwa vita vya biashara utavunja kina cha uhusiano wa ulinzi kati ya Marekani na maadui wake wa msingi wa vita vya pili,ambao ni washirika wake kwa miaka 40 iliyopita.

Wamarekani wanapaswa kuandaan kushuhudia kuibuka kwa Wajapani waliojihami na zana za nyuklia-muungano wa Ulaya na Ujerumani walijihami na silaha na viini vyake.Kuna shaka kama raia wa Marekani na wawakilishi wao waliochaguliwa wamefikiria matokeo ya matendo yanayoendelea sasa hivi.

Kiongozi wa Seneta anayewakilishi wengi Howard H.Baker Jr.alitoa onyo hili: "Muswada wa Ushuru wa hatari ya Smoot-Hawley ya 1930 ulipitishwa haraka na Kongamano...na ilichukua miaka 14 na vita vya ulimwengu kulainisha fujo." (Hogberg G.Prepare for Trade War! Plain Truth,Januari 1986)

Tena,wakati kutabiri kwake ni mapema,matukio yanaelekea kwa yale aliyoyaandika.Tangia wakati aliandika haya Yuro imeonekana katika eneo la ulimwengu (kana kwamba inachukua

nafasi) na itatumika badala ya dola ya Marekani kama sarafi hifadhi ya ulimwengu.

Tazama niliyoandika hapo awali mnamo mwaka wa 2008:

Mazungumzo yataendelea na aina ya makubaliano yasio thabiti yatafanyika.Katika hali ya maafikiano na nia ya kibinagsi, "viwango" vingi vya Umoja wa Ulaya vitatumika na Marekani,Kanada na Meksiko,na hata karibia nchi zote za ulimwengu.Mataifa ya Warabu watakubaliana na viwango vingi kwa sababu wanaonekana kuunda muungano wa nyakati za mwisho na Wazungu.

Hata hivyo,baada ya muda mchache,itaonekana wazi kwamba Waingereza watakuwa na makubaliano na Wakanada na Wamarekani na kwamba Umoja wa Ulaya utakuwa na makubaliano na Wameksiko kuliko vile Umoja wa Ulaya ungekuwa nayo na mataifa yanayozungumza Kiingereza.

Vita vya biashara na/ama mgogoro wa ajabu utachipuka.

Waingereza hatimaye wataamua kwamba wanaunga Wamerika na Wakanada sana.Wataungana mikono kiasi kwamba watafikia makubaliano nao(na Wa Australia na Wanyuziland pia wanaweza kuwa sehemu ya makubaliano).

Muungano wa Ulaya wataamua kwamba Meksiko na Wamarekani wa Kilatini wengine wanakuwa katika makubaliano zaidi naye kwa hivyo watafanya aina ya makubaliano ya ajabu ya biashara na wengi (ama wote)

wa Latini Wamarekani.Vatikani pia watakuwa na ushawishi hapa kama Marekani wa Latini wengi wao ni Wakatoliki.

Wazungu na Wamarekani,hata hivyo,wataendelea kuwa na uhusiano wa kivita,hata hivyo wengi watawaogopa.(Thiel B.A combined EU & North American Trade Block Coming? COGwriter.com,March 3,2008).

Vita vya biashara vinaongeza gharama na wasiwasni wa kimataifa.

Inafaa ikumbukwe kwamba kulingana na maongezi ya kikwazo kutoka kwa Rais wa Marekani Donald Trump,katika mwisho wa 2017,China,Urusi na Venezuela walianza kuchukua hatua kuacha kutumia dola kama sarafu hifadhi ya kimsingi.Kupotea kwa dola ya Marekani kuwa sarafu ya hifadhi kutauimiza uchumi wa Marekani kwa njia nyingi.Wakati tendo hili halitatokea mwaka wa 2018,migogoro/vikwazo vinasukuma mbali sana ulimwengu kutoka kwa dola ya Marekani.

Zaidi ya hayo,kulingana na uchaguzi wa Uingereza kujiondoa kutoka kwa Umoja wa Ulaya (Unayoitwa Brexit) na uchaguzi wa Donald Trump kuwa Rais wa Marekani,imeleta utengano mkubwa kutoka kwa Ulaya,Marekani na Uingereza sote wanatafuta uhusiano wa kibashara kati yao.Meksiko wanaangalia Ulaya.Ulaya inaangalia Amerika ya Kusini na Asia.

Tazama kifungu kimoja kutoka kwa vyombo vya habari vya Ujerumani:

Ulaya lazima wawe tayari kutafuta mshirika mpya wa kiuchumi katika Asia wakati Rais anaharibu kiungo kinachokuwepo cha ulimwengu cha

utaratibu wa uchumi.(Riegert B.The EU has to stand up to Donald Trump.Deutsche Welle,January 31,2017).

Kwa vile hali ilivyo,hii imefanyika.Katika 2017,Ulaya,hasa,viongozi wa Ujerumani walikuwa wakiunda biashara wakati Marekani waliacha kushirikiana katika Mkataba Mchanganyiko wa Ushirika wa Pasifikasi na wakachukua hatua zingine dhidi ya mipangilio mingine ya biashara iliyokuwepo.

Taarifa ya Rais wa Marekani Donald Trump kwa Umoja wa Mataifa kuhusu biashara na "Wamarekani kwanza" mnamo Septemba 19,2017,pia ilionyesha sehemu ya ulimwengu kwamba Marekani wanataka kubadilisha utendaji wa biashara katika njia ambazo mataifa mengi hawaamini kama zitawaletea faida-na hii inasaidia kuufungua mlango kwa Umoja wa Ulaya.

Tena,viongozi wa Ulaya wamesema kwamba hawataki waendelee "kuwa chini ya" Marekani na wanataka waweke "Ulaya kwanza" (tofauti na kauli mbiu "Marekani kwanza" ambayo Donald Trump alikuwa akitumia wakati wa kampeni.)

Kulingana na vile kuwa chini ya amri inavyoenda,viongozi wa Ulaya wanagundua kwamba wamekuwa chini ya amri ya Marekani kwa vile wametegemea majeshi ya Marekani kwa ulinzi tangia mwisho wa vita vya ulimwengu wa II katika Ulaya Magharibi,na pia baada ya kuanguka kwa ukuta wa Berlin,na ulinzi wa kijeshi katika Ulaya Mashariki na Baltiki.

Ulaya sasa wanataka kuimarisha jeshi lao,huku wakiongeza biashara ya kimataifa.Ulaya wanataka kuweka viwango kwa bidhaa vingi na

huduma na pia sheria ya biashara nyingi ya ulimwengu.

Mnamo mwaka wa 2017,Umoja wa Ulaya walikuwa na mikutano na Meksiko na wengine kama Marekani wa Kusini kujadili masuala ya kibiashara mara nyingi.Waziri Mkuu wa Ujerumani Merkel pia alienda Ajentina kuweka misingi ya mikataba ya biashara na taifa hilo pamoja na Meksiko.Kulikuweko na mikutano na safari kwenda Urusi,China na mataifa mengine.

Biblia ni wazi kwamba Ulaya itainuka kuwa na jeshi kubwa na ulimwengu utashangaa (Ufunuo 13:1-10;Danieli 11:39-43) na nguvu zaidi ya kibiashara (Ufunuo 18).

Katika majira ya kiangazi ya 2017,Kongamano la Marekani walipitisha sheria ya kuongeza vikwazo dhidi ya Urusi.Washirika wake wa Ulaya waliwaonya dhidi ya kufanya hivyo,lakini wakaendelea kuiweka kama sheria.

Waingereza walijaribu kuwaunga mkono katika msimamo wao,lakini wale walioko Ulaya hawakuwaunga.Ulaya walionya muswada wa vikwazo utaleta vita vya kibiashara-vita vya kibiashara ambavyo viongozi wengine wa Umoja wa Ulaya wanadai kwamba Ulaya ndiyo itashinda.

Wakati mataifa kwa kawaida hawashindi vita vya biashara,viongozi wa kisiasa wamepata jambo hili la muhimu sana kwa sababu nyingi.

Masuala ya kibiashara ni muhimu na yanaenda sambamba na unabii wa mwisho wa Kibiblia.

Matukio katika Marekani na Ulaya yanafungamana na kuelewa kwa unabii wa kibiblia ambayo sisi katika Kanisa la Mungu *Linaloendelea* linashindania na kuyafunza.

Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea "tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi,ambalo mkiliangalia,kama taa ing'aayo mahali penye giza,mwafaka vyema,mpaka kutakapambazuka,na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu" (2 Petro 1:19,KJV).

## **Je! Uko tayari kuila Pasaka?**



***Usiku wa Pasaka unahusisha Mkate usiotiwa chachu na mvinyo wa divai***

Na Albert J.Portune

***Hii nakala ilichapishwa awali katika Jarida la Habari Njema,Machi 1969 (na maandiko yaliyonukuriwa yalibadilishwa kwa NKJV badala ya KJV)***

Pasaka ni ukumbusho wa kifo cha Yesu Kristo ambaye ni Mwokozi wa ulimwengu.Kushiriki kwa ishara ya mwili uliovunjwa na damu iliyomwagika inamaanisha kwamba umechaguliwa kujua na kuelewa kusudi la Mungu.Kwa kuchaguliwa kama moja ya WATEULE ili ujue ukweli wa Mungu kunabeba kiasi cha majukumu.Hatuwezi kukaribia tukio hili kwa wepesi.

### **Mwanzo wa Sikuu**

Pasaka ni tukio la kwanza linaloanza tena msimu wa mwaka wa msimu wa Sikuu.Sikuu zake zinafunua mpango wa Mungu wa wokovu wa ulimwengu wote.Mpango huo,ambao haujulikani na ulimwengu kwa jumla,unaonyesha kwa nini huwezi kuchukua tukio hili kwa wepesi.

Mpango huo unaonyesha kwamba umeitwa kujua na kuelewa kusudi la Mungu-KABLA ya watu wengi kujua.Yesu alisema:

Akajibu,akawaambia,Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni,bali wao hawakujaliwa.(Mathayo 13:11)

Ulimwengu hawaitwi sasa! Wateule pekee ndio wanaitwa.Sikuu za Mungu,ambazo zinafanyika wakati wa misimu ya kuvuna katika Palestina,zinaonyesha kwamba sisi ni sehemu ya mavuno ya awali-yaani wateule.Malimwengu wengine hawatapewa nafasi hadi Kristo arudi na miaka elfu ianze-yaani majira ya mwisho wa majani kupukutika-(tazama Walawi 23).

Ukweli wazi ni kwamba tumeitwa katika wito maalum ama tumepewa nafasi ya kuhitimu mbele ya ulimwengu ili tutumike na Mungu na Kristo kwa kuleta maarifa na wokovu kwa ulimwengu mzima.

Mungu anatuangalia sana tunapokaribia Pasaka hii,kwa sababu ya sehemu yetu katika Mpango wake.Anajali sana mtazamo wetu.Anataka kujua ikiwa tumejitolea kwake.Kwa hivyo ni wakati wa kujichunguza ili tuone kama tumekuwa sawa mbele ya Mungu na kuwa na amani kwa Mungu na mpango wake.

### **Kujihoji Mwenyewe**

Je! Unajua kwamba katika Pasaka hii inayokuja unaweza kula na kunywa HUKUMU? Je!  
Unagundua jinsi ni hatari kufanya hivyo?

Mungu alitia msukumo Mtume Paulo kuandika:

27 Basi kila aulaye mkate huo,au  
kukinywea kikombe hicho cha Bwana  
isivyostahili,atakuwa amejipatia hatia  
ya mwili na damu ya Bwana.28 Lakini  
mtu ajihoji mwenyewe,na hivyo aule  
mkate,na kukinywea kikombe.29  
Maana alaye na kunywa,hula na  
kunywa hukumu ya nafsi yake,kwa

kutopambanua ule mwili.( I Wakorintho 11:27-29).

Ndugu wapenzi, onyo hili halingekuwa katika Neno la Mungu ikiwa hakuna hatari KWAKO. Pasaka hii inayokuja ni wakati muhimu, hata kama umeshiriki Pasaka mara nyingi ama unaenda kushiriki mara ya KWANZA.

Ni nini maana ya kupambanua mwili wa Bwana? Je! Twavezaje kumla na kunywea isivyostahili? Twavezaje kumla na kunywea hukumu kwetu? Wacha tuelewé.

### **Kuingia katika mwelekeo**

Mungu anataka tujitenge mtazamo wa msingi kila mwaka wakati wa Pasaka. Anatuhitaji tupate mwelekeo kwa dhana hii ya kimsingi tukianza tena kuishi katika mpango wake wa kuokoa binadamu. Dhana hii ya kimsingi ni wokovu. Mpango wake unahuhiyo hata kama inahusiana nasi ama ulimwengu.

Kwa hivyo, ndugu zangu, Pasaka ni wakati ambapo twafaa tuangalie tena mafundisho ya wokovu WETU-uhusiano WETU kwa Mungu na Kazi yake. Ni wakati wa kujihoji WENYEWE. Wakati wa kujiangalia MWENYEWE.

Twaweza kutekwa sana katika kazi zetu ama katika "vitu vya ndani," vitu muhimu sana, kiasi kwamba twasahau kwamba twapaswa kuwa wema mbele za Mungu. Hiyo ndiyo Pasaka inahusu.

Hakuna wakati tunaweza kusema kwamba tumekuwa na shughuli sana ama tumekuwa muhimu sana usoni mwetu kiasi kwamba tunasahau kuwa twapaswa kuwa makini zaidi kuhusu dhana ya kimsingi ya wokovu ambazo zinahusiana na Pasaka.

### **Kanuni za Kimsingi**

Haijalishi tumedumu muda mrefu katika Kanisa la Mungu ama jinsi tumekuwa watu wa kiroho bado sisi ni wanadamu ambao wana tabia ya binadamu. Hakuna mtu ye yote anaweza fikia mahali po pote katika maisha haya ambapo tunasahau jinsi tulivyo. Kabla ya Pasaka twapaswa kujiangalia-uangalivu mrefu, mzuri!

Ni jinsi gani Mungu alituumba?

Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani aezaye kuujua? (Yeremia 17:9)

Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. (Warumi 8:7).

Ndiyo, hiyo ndiyo aina ya nia Mungu (aliruhusu iwekwa) ndani yako! Na huu ndio wakati wa mwaka hasa wa kukumbuka ukweli huu. Pia ni wakati wa kukiri na kuthibitisha kile umefanya na maarifa uliopewa kujuia kwamba una aina ya nia hiyo. Ukweli ni kwamba Mungu aliumba nia iliyotengana naye na njia zake. Moyo wa mwanadamu umeinuka kwa maovu. Ni mdanganyifu, na unapinga sana njia za Mungu. Watu wengi hawajajiona hivyo. Watu wengi hawajui hata kidogo kwamba wana aina ya nia kama hii-lakini ni ukweli wanayo.

### **Mazingira Pia**

Sio kwamba nia ya binadamu iko hivyo, lakini mazingira yake pia hayapatani kabisa na Mungu. Mwanadamu hajui kabisa kwamba ulimwengu huu bado sio ulimwengu wa MUNGU. Mungu anamruhusu Shetani atawale kwa muda. Anaruhusu Shetani kuwadanganya wanadamu kupitia kwa nia mbaya na potofu ambayo inataka na kuhifadhi maovu yote ya ulimwengu huu.

Shetani ndiye mtawala wa ulimwengu kwa wakati huu na anapofusha akili za watu ili wasijue ukweli kwamba umepewa nafasi ya kuelewa.

"Lakini ikiwa injili yetu imesitirika,imesitirika kwa hao wanaopotea;ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini,isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu." (II Wakorintho 4:3-4)

"Maana kile kilichomo duniani,yaani,tama ya mwili,na tama ya macho,na kiburi cha uzima,havitokani na Baba,bali vyatokana na dunia" (I Yohana 2:16)

Kwa hivyo,kwa kujihoji,wacha tutambue jinsi nia yetu inajitenga na aina ya ulimwengu tunamoishi ndani mwake.

### Nuru katika Giza

Lakini,ndugu zangu,sisi ni Wateule,nuru na kuelewa imekuja kwa wito wa Roho Mtakatifu wa Mungu.Kwa kuitia kwa rehema usio na mpaka ambayo umeitwa kama mmoja wa Wateule ujione na kutazama mazingira jinsi yalivyo!

Hii ilikuwa miujiza katika maisha yako! Je bado unatambua hivyo?

Mungu alituma Roho Mtakatifu kufungua akili yako ujue maarifa kamili.Kitu cha kwanza alifungua wazo lako ujue ni wewe MWENYEWE! Uliogozwa kuona vile nia ya binadamu inavyofanana-jinsi ulivyokuwa.

Haukupenda ulichokiona!

Ulitaka kuwa tofauti.Kwa hivyo ukafikia toba-mabadiliko kwako mwenyewe-kwa sababu hiyo

ndiyo toba.Maneno ya Mtume Paulo yakawa maneno yako: "kwa sababu lile nilipendalo,silitendi,silitendi;bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda,ndani ya mwili wangu halikai neno jema;kwa kuwa kutaka nataka,bali kutenda lililo jema sipati.Ole wangu maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? (Warumi 7:15,18,24.)

Kwa hivyo ulifikia toba na ukabatizwa.Ulipitia MFANO wa nje wa kifo.Ubatizo ni ishara ya kifo,kuzikwa na kufufuka.Ulitumbukizwa katika kaburi ya maji na kuinuliwa juu katika aina ya ufufuo.

4...sisi tuliofia dhambi tutaishije tena katika dhambi?3 Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? 4 Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake,kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba,vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.(Warumi 6:2-4).

Baada ya kujiona jinsi ulivyokuwa,ulitaka kuacha kuwa adui wa Mungu.Ukahitaji kukomesha kuwa mrongo,mwovu.Ulitaka matendo maovu yote ya awali na fikra ziondolewe mbali.Ulitaka kuwa mpya na mtu tofauti.Ulionwa kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili yako.Ukaona kwa nini angekufa-ili ali pe gharama ya dhambi zako,kwa sababu ya nia yako potofu.Kwa hivyo ukamtambua Yesu kama Mwokozi wa maisha yako.Ukamwuliza Mungu akubali dhabihu ya maisha ya Yesu Kristo kwa sababu ya dhambi zako na nia yako iliyooza.Ulimwonyesha Mungu waziwazi kwa njia ya ubatizo ulichotarajia-ili nia yako maovu ife na kubadilishwa kuwa aina ya nia ambayo siyo adui wa Mungu.

Mungu alipoona mtazamo wako wa kweli kutoka moyoni, alikupa Roho Mtakatifu na ukakombolewa kama mtoto wake.

### **Syo Mwisho**

Lakini hiyo siyo mwisho wa hadithi! Sasa pengine inaanza sehemu ngumu sana, baada ya kusulubisha "nia ya awali," twapata tena kwamba nia ya awali haikuwa. Hata hivyo tulitamani kwamba nia hiyo iharibike, tulipata kwamba bado ina uzima na nguvu.

NA HIYO NDIYO HOJA!

Mungu alifanya hivyo kwa kusudi muhimu. Mungu anataka tufahamu KINA HALISI CHA MAOVU, MABAYA NA UDANGANYIFU yaliyo ndani yetu. Mungu anaruhusu tuishi na tabia yetu ya kimwili na katika mazingira ya kigeni ili tuweze kufundishwa jinsi nia ya mwanadamu ni maovu-na anataka tukubaliane naye kwamba kuna maovu-kupitia kwa uzoefu wa maisha yote ya Ukristo.

Twajua kwamba tumesulubisha utu wetu wa kale kiasi kwamba mwili wa DHAMBI(nia yetu halisi) iweze kubatilika (Warumi 6:6). Twajua kwamba tutakopofufuliwa ama kubadilishwa wakati wa kurudi kwa Yesu, tuondolewa aina hiyo ya nia (mstari wa 7). Lakini, hadi wakati huo ufile, lazima tujihesabu kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa maisha ya haki (mstari wa 11). Mapambano basi yaanza wakati "dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake" (mstari wa 12).

Kwa, hivyo tunapokaribia Pasaka, tunao mwaka mmoja wa kuishi pekee yetu. Mungu sasa anatuuliza tena tushiriki kwa mwili wa Kristo uliovunjwa na damu yake iliyomwagika. Je mwaka huu uliopita umekushawishi kwamba umekuja mahali ambapo hauhitaji tena dhabihu ya Kristo? Ama umekushawishi kwamba

unahitaji KWA KINA sana dhabihu kuliko vile ulivyohitaji hapo awali?

HII NDIYO MAANA YA KUPAMBANUA MWILI WA BWANA.

Bila shaka umekua katika kukabiliana na dhambi. Bila shaka umekua katika kuelewa na katika maarifa ya kiroho. Lakini je, umekua katika kujuwa kwamba unahitaji Yesu Kristo kuliko vile ulivyomhitaji awali?

### **Kuangaliwa kwa Kina?**

Wakati tulibatizwa mara ya kwanza tuliiwa "watoto wachanga" katika Kristo. Pamoja na hayo, tumefikia miujiza na maarifa ya kina wakati wa batizo, lakini bado tunaanza maisha ya kushinda. Tunahitaji kukua na kukomaa katika kuelewa na mtazamo.

Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpare kuukulia wokovu (I Petro 2:2)

Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. (II Petro 3:18)

Tunapokua katika maarifa ya kina ya vitu vya kiroho uwezo wetu wa kujiona wenywewe unakuwa kubwa. Tunaona mambo yanayotuhusu na utu wetu ambao hatukuona wakati wa batizo. Hiyo ni sawa! Ni maendeleo! Hiyo ndiyo Mungu anatarajia.

Wakati Paulo alipokea Roho Mtakatifu wa Mungu na akaanza kukua alipata kwamba maarifa yake ya kina ya amri ya Mungu ilifanya dhambi inaonekane kuwa mbaya mno (Warumi 7:13). Na pia nasi twahitaji kuwa hivyo. Kadri tunavyozidi kuishi na nafsi yetu katika mwili wetu ndivyo tunavyozidi kujuwa sheria ya Mungu

ya kiroho,ambayo tuna bahati kuelewa,na inatutia hatia zaidi kwa utu wetu wa kimwili uliojawa na dhambi.

Kila mwaka Mungu anatuamuru tuishi tena kupitia Sikukuu zake ambazo zinaonyesha mpango wake wa kuokoa ulimwengu.Kila mwaka tunaanza tena na mwanzo wa kimsingi-Pasaka-kukubali dhabihu ya Yesu Kristo.

Kila mwaka twapaswa kuadhimisha Sikukuu za Mungu kwa hamu kubwa ya kutimiza mpango wake kwa sababu tumeona umuhimu wake kwa kina kuliko tulivyoona awali-kwa ajili yetu na kwa ajili ya ulimwengu.

Tunapoanza Sikukuu tena inafaa tuanze na shauku upya.Inafaa iwe na hamu ya dhati kuchukua mfano wa thamani kubwa kwa sababu twajua sana maana zao kwetu sisi na kwa ulimwengu.

Hii siyo utaratibu wa kawaida ambayo tunaanza kila mwaka.Hatuwezi kukaribia siku hizi kwa moyo ambaao haujali.Tukifanya hivyo twaweza kula na kunywea "isiyofaa"-kula na kunywea hukumu kwetu.Hakuna mtu "anayestahili." Kuelewa kinagaubaga jinsi hatustahili dhabihu kuu ya Kristo,inatufanya tuwe tayari kushiriki Pasaka kwa ufahamu kamili!

Mungu anataka watu wake wafikie Pasaka na hamu ya dhati na hodari ya msamaha wa Kristo-waje kila mtu peke yake na baadaye kwa ulimwengu.Hakuna mtazamo wo wote unaoonyesha Mkristo ambaye amekua kama inavyotastahili kwa mwaka mzima.

#### JE! UKO TAYARI KUSHIRIKI PASAKA?

Hakuna mtu ye yote ambaye ameishi mwaka mzima katika mwili na uwepo wa Roho Mtakatifu anaweza kufikia Pasaka bila haja ya kina kwa dhabihu ya Kristo.Kwa hivyo hakuna

mtu atakayeshiriki mkate usiotiwa chachu wa mwili wa Yesu na divai ya damu yake iliyomwagika bila kuanguka kwa roho mbele ya msalaba mbele ya mwili wa Yesu unaotoka damu,unaokufa na kusema " Amekufa kwa ajili yangu,ewe Mungu,ulikufa kwa ajili yangu!"

**19 Akatwaa**  
mkate,akashukuru,akaumega,akawapa akisema, (Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu;fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.20 Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula;akisema,Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwagika kwa ajili yenu.(Luka 22:19-20).

Haya maneno yanafaa kuwa hai na ya kipekee kwako kuliko vile yalivyo awali.JE! YAMEKUWA HIVYO?

#### Taswira Kubwa

Baada ya kuwa na mahitaji ya kipekee kwa dhabihu ya Yesu Kristo katika maisha yako,twapaswa tuwe na haja kubwa na ya ndani kwa ukweli huo na ufahamu wa kufikia ulimwengu huu ulio mgonjwa na uliopotea.Siyo kwa nadharia bali kwa hakika.

Tunaanza tena na Pasaka,inayoonyesha mpango wa wokovu wa ulimwengu.Sio wokovu wako peke yako.Kuna maisha ya wanadamu wengi ambaao wako karibu nasi wanaopotea.Kupoteza matumaini kwa sababu ya ustaarabu unaokufa unatupatia uchungu katika mawazo yetu kila siku.

Sisi tuliopewa maarifa ya njia PEKEE ya kuokoka kwa ulimwengu tunapaswa kuhisi uchungu ndani yetu ili na wao pia wafike wakati watatolewa kutoka kwa utumwa wa ujisadi ambaao tumefanywa tuujue.Kila mwaka mpya wa maadhimisho ya Sikukuu unafaa uwe katika

kiwango cha kutambua na maana kubwa ya  
dhati ya utimilifu.

Kuna KAZI MOJA ambayo inafanywa mpaka  
mwisho...NI KAZI HII.Na wewe ni sehemu ya kazi  
hiyo.

Je! Mwaka huu uliopita umekuleta katika  
kujitolea kwa undani? Je,unafanya Kazi ya  
Mungu na maisha yako yote na yote unayo?  
Ama Sikukuu za kila mwaka ni utaratibu wa  
kawaida kwako tena?

16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda  
ulimwengu,hata akamtoa Mwanawe  
pekee,ili kila mtu amwaminiye  
asipotee,bali awe na uzima wa  
milele.17 Maana Mungu hakumtuma  
Mwana ulimwenguni ili auhukumu  
ulimwengu,bali ulimwengu uokolewe  
katika yeye.18 Amwaminiye yeye  
hahukumiwi;asiyeamini amekwisha  
kuhukumiwa;kwa sababu hakuliamini  
jina la Mwana pekee wa  
Mungu.(Yohana 3:16-18)

Ikiwa umeamini katika kusudi la Mungu kupitia  
kwa Yesu Kristo na UKO TAYARI kwa kusudi hilo  
KATIKA MAISHA yako,basi unapambanua mwili  
wa Bwana na unakula na kunywea uzima wa  
milele.Lakini ikiwa maisha yako na matendo  
yako yanaonyesha kazi ya udhaifu bila kujitolea  
kwa kazi ya Mungu-unakula na kunywa hukumu  
kwako-bila kupambanua,bila kuelewa maana  
kamili ya mwili wa Bwana.

JICHUNGUZE!

### **Uifanye binafsi**

Ndugu zangu,bado kuna muda wa kujichunguza  
na kuifanya Pasaka hii kama kitu cha binafsi kati  
yako na Mungu.Angalia kwa makini maisha  
yako.Je,unaenda tu bila nguvu? Je,ulikuwa

unaenda tu kufanya Pasaka hii iwe Pasaka ya  
kawaida? Kama haya ni ukweli basi unahitaji  
sana dhabihu ya Yesu Kristo kwa uzembe  
ambao Roho wa Mungu amekuongozwa uone  
kwako-kama vile ungepaswa kuongozwa ili  
uone vitu vingine vinavyokuhusu katika mwaka  
uliopita.

Kwa kila Mkristo anayekua,kila Pasaka inafaa  
iwe uzoefu wa kina ambapo Mwokozi wetu na  
Mungu wetu anakuwa mahususi  
kwako,mwenye thamani kubwa,na wa ajabu  
sana.

**JE UKO TAYARI KUSHIRIKI PASAKA-JE,UTAKUWA  
TAYARI?**

Wakati wa chakula cha jioni hiyo ya Pasaka,Yesu  
alisimama na akatwa kitambaa,akajifunga  
kiunoni ,akaanza kuwatawadha miguu ya  
wanafunzi wake (Yohana 13:2-5).Petro akiwa na  
msisimko bila kujua,hakutaka Yesu ainame na  
kutawadha miguu.Lakini Yesu akamwambia,  
"Kama nisipokutawadha,huna shirika nami"  
(Yohana 13:8) Petro,kwa ukweli alikuwa akitaka  
kuwa mshirika na Kristo na akakubali.

Yesu basi akasema:

12....Je! Mmeelewa na hayo  
niliyowatendea? 13 Ninyi  
mwaniita,Mwalimu,na,Bwana:nanyi  
mwanena vema,maana ndiyo nilivyo.14  
Basi ikiwa mimi,niliye Bwana na  
Mwalimu,nimewatawadha miguu ninyi  
kwa ninyi.15 Kwa kuwa nimewapa  
kielelezo;ili kama mimi  
nilivyowatendea,nanyi mtende vivyo.16  
Amin,amin nawaambia ninyi,Mtumwa si  
mkuu kuliko bwana wake;wala mtume  
si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.17  
Mkiyajua hayo,heri ninyi  
mkiyatenda.(Yohana 13:12-17)

Tutatawadhana miguu siku ya Pasaka.Lakini tena inaonyesha ishara ya nje ya tabia na matendo katika maisha yetu-tabia ya kuhudumia kina ndugu na kujitolea katika UNYENYEKEVU kwa makusudi ya Mungu.

Je,uko na sehemu yako katika Yesu Kristo? Je! Uko katika mtazamo wa kutawadha miguu KILA MWAKA.Hyo ndiyo maana kamili ya ishara ya kutawadha miguu utakayoshiriki.Je,unapambanua Mwili wa Bwana? Ama umekuwa kama Petro-ambaye hakutaka makusudi ya Mungu yatendeke kwake ili awe kama mtumishi.Mkristo anayekua,anayepambanua anajua kwamba ameitwa na Mungu ili ajinyenyekee kama mtumishi wa kina ndugu na wanadamu wote.

#### **Wakati ni Sasa**

Kwa hivyo,ndugu zangu,wakati ni SASA.Pasaka i mbele yako.Umekuwa na mwaka mwingine wa kuishi,kupata uzoefu na kukua.Mandhari ya MAISHA YAKO yanapatikana mbele yako pamoja na uwakilishaji wa dhabihu ya Kristo.

3 Alidharauliwa na kukataliwa na watu;  
Mtu wa huzuni nyingi,ajuaye sikitiko;  
Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao,

Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.

4 Hakika ameyachukua masikitiko yetu,  
Amejitwika huzuni zetu;  
Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa.  
Amepigwa na Mungu na kuteswa.  
5 Bali alijeruhija kwa makosa yetu;  
Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake,  
Na kwa kupigwa kwake sisi  
tumepona.(Isaya 53:3-5)

**UWE TAYARI KWA KUSHIRIKI PASAKA!**

#### **Usiku wa Kuangaliwa na Siku za Mkate Usiotiwa Chachu**



#### **Mkate Usiotiwa Chachu**

Na Bob Thiel

Pasaka ni siku ya 14 ya Nisani ama Abibu.Katika mwaka wa 2018 kwa kalenda ya Rumi,Pasaka itaadhimishwa baada ya machweo ya tarehe 29 Machi.Wakati watu wengi wanafahamu Pasaka,wengi hawafahamu "Usiku wa Kuzingatiwa" (ambayo inaadhimishwa baada ya machweo ya Machi 30 wa mwaka wa 2018) na Siku ya Mkate Usiotiwa Chachu.Kwa hivyo makala hii italenga hayo.

Kristo ndiye Mwanakondoo wa Pasaka ( 1 Wakorintho 5:7) ambaye alituokoa kwa dhambi (Warumi 6:17).Biblia pia inaonyesha kwamba Misri ni aina ya dhambi ambayo wana wa Israeli walitoka na wakaokolewa (Kutoka 13:3;Ufunuo 11:8).Biblia inaonyesha ya kwamba Wakristo leo hii wanaishi katika ulimwengu ambao ni aina ya "Babeli" ya kiroho (Ufunuo 17:1-6).

Biblia inoanyesha kwamba hivi karibuni Wakristo wataokolewa kutoka kwa Babeli baada ya Mungu kumwaga mapigo yake kwa Babeli (Ufunuo 18:1-8).Mapigo mengi ambayo yameorodheshwa katika Kitabu cha Ufunuo yanafanana na yale yaliyotumika Misri kabla watu wa Mungu hawajaondolewa.

Wana wa Israeli walitoka Misri siku ya Kwanza wa Mkate Usiotiwa Chachu.

Biblia,katika Mambo ya Walawi 23:7-8

inafundisha kwamba siku ya kwanza na ya mwisho wa mkate usiotiwa chachu ni wakati wa "kusanyiko takatifu".Jioni ya siku ya kumi na tano ya Nisani (ambayo inaanzia sikuu hiyo ndiyo mwanzo wa Sikukuu Usiotiwa Chachu,ambazo ni siku za mlo (Kutoka 12:16;Walawi 23:6).

Biblia inarekodi yafuatayo:

<sup>42</sup>Ni Usiku wa kuangaliwa sana mbele za BWANA kwa sababu ya kuwatoa katika nchi ya Misri;huu ndio usiku wa BWANA,ambao wapasa kuangaliwa sana na wana wa Israeli wote katika vizazi vyao.(Kutoka 12:42 KJV)

<sup>42</sup>Huu ni usiku wa kuangaliwa mbele za BWANA,ambapo aliwatoa katika nchi ya Misri:Usiku huu wana wa Israeli wote lazima waadhimishe katika vizazi vyao vyote.(Kutoka 12:42,Douay Rheims wa awali)

Kwa Wakristo,Usiku wa Kuangaliwa unaonyesha kuchukua hatua kwetu kutoka kwa Misri ya kiroho ( Ufunuo 11:8)-hiki ni kitu ambacho kinafaa kifanye Wakristo washangilie.

Kihistoria,Usiku wa Kungaliwa kawaida unakuwa sherehe ya mlo mkuu wa jioni.Mlo huo ulikuwa na Mkate usiotiwa chachu.

#### **Wayahudi Wengi Wanaiita siku ya 15 Pasaka**

Viongozi wa Wayahudi walibadilisha tarehe na desturi zinazohusiana na Pasaka.Vyanzo vingine vya rabii vinapendekeza tarehe hiyo kwa sababu hawataki kuadhimisha siku hiyo vile Wakristo waaminifu wanavyofanya.(Wolf G.Lexical and Historical Contributions on the Biblical and

Rabbinic Passover.G.Wolf,1991).Lakini pia,kwa sababu ya kukila usiku wa Kuangaliwa na

desturi zingine,ukiunganishwa na jinsi Wayahudi walikuwa wakikabiliana na sikukuu kwa sababu ya ugenini (Wayahudi waliokuwa nje ya Israeli) na masuala ya Kalenda (Holy Days.Jewish Encyclopedia of 1906),Wayahudi wanajaribu kuiita Siku ya Kuangaliwa kama Pasaka kwa sababu Wayahudi wengi wanaidhimisha tarehe 15 kama Nisani/Abibu.Wengine wanaidhimisha tarehe 14 na 15 kama Pasaka.

Wakati wa Yesu,Masadukayo walijaribu kuadhimisha Pasaka katika siku ya 14 na Mafarisayo waliadhimisha siku ya 15 kama Pasaka.

Wakati wa Yesu,Masadukayo walikuwa wakiadhimisha Pasaka siku ya 14 na Mafarisayo waliaadhimisha Pasaka siku ya 15 (Rabii Jeffrey W.Goldswasser.Why do Jews in America have two Passover Seders?)

Kwa hivyo,Biblia inafundisha kwamba nyakati mbili hizi zina makusudi tofauti.Pasaka ya Agano la Kale inaonyesha kwamba wana wa Israeli walilindwa na hawakuaribiwa na malaika wa kifo.Pasaka ya Agano Jipya inaonyesha Wakristo kwamba Yesu aliibeba adhabu ya dhambi zetu pekee yake kuitia kifo chake.

Lakini Usiku wa Kuangaliwa inakumbusha Wayahudi kwamba wanapaswa kushukuru Mungu kwa kuwatoa kwenye kifungo cha utumwa wa Misri (Kutoka 12:42).Kwa Wakristo,Usiku wa Kuangaliwa unatufundisha kwamba tunapaswa kufurahi na kushukuru kwa uhuru Yesu ametupatia kutoka kwa utumwa wa dhambi(Yohana 8:34-36).

Wasomi wengine wa Wayahudi wanajua kwamba Biblia inaonyesha Pasaka kuwa katika tarehe tofauti na Sikukuu za Mkate Usiotiwa

Chachu.

Walawi xxiii,hata hivyo,inaonekana kutofautisha kati ya Pasaka,ambayo imetengwa katika siku ya 14 ya mwezi,na (Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu;Luka xxii.1;Yusufu, "B.J" ii.1,& 3),iliotengwa kuwa siku ya kumi na tano ya mwezi huo.(Passover.Jewish Encyclopedia of 1906)

Kwa hivyo,lichu ya Wayahudi kuadhimisha wanachokiita siku ya 15 ya Pasaka,siku ya kumi na tano,kibiblia inazingatiwa kuwa sehemu ya siku saba ya Siku za Mkate Usiotiwa Chachu.Kwa sababu Wayahudi wanajaribu kusisitiza kutoka huko Misri na wanategemea mapokeo yasiyo ya kibiblia,wanajaribu sana kuadhimisha tarehe ya pili ya Siku ya Mkate Usiotiwa Chachu.

Kutoka 12 inafafanua Pasaka na inaanza na Mungu akiagiza Musa na Haruni kuhusu wanachotakikana kufundisha watu na pia kitakachotokea.Maagizo ni pamoja na kumtwaa mwanakondoo siku ya kumi ya mwezi wa kwanza,unaoitwa Abibu,na kumtunza hadi siku ya tarehe kumi na nne wakati angeuawa jioni-kuanzia tarehe 14.

Tazama jambo fulani kutoka kwa maagizo yafuatayo kuhusu Pasaka:

<sup>21</sup>Hapo ndipo Musa akawaita wazee wa Israeli,na kuwaambia,Nendeni,mkajitwalie wana-kondoo kama jamaa zenu zilivyo mkamchinjie pasaka.<sup>22</sup>Nanyi twaeni tawi la hisopu,mkalichovye katika ile damu iliyo bakulini na kukipiga kizingiti

cha juu,na miimo miwili ya mlango,kwa hiyo damu iliyo katika bakuli;tena mtu ye yote mionganoni mwenu asitoke mlangoni mwa nyumba yake hata asubuhi.(Kutoka 12:21-22)

Usemi "hata asubuhi" unatoka kwa neno la Kiyahudi linalomaanisha "kupambazuka",au "maawio ya juu" ama "kulipokucha."

Kwa Waisraeli hawakuondoka nje mpaka kulipobambazuka tarehe 14.Ni nini ilifanyaika usiku huo?

<sup>29</sup>Hata ikawa,usiku wa manane BWANA akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri,tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi,hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa;na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama...<sup>33</sup>Wamisri nao wakawahimiza watu,kuwatoa katika nchi kwa haraka,maana walisema,Tumekwisha kufa zote.(Kutoka 12:29.33)

Musa na Haruni hawakuondoka nje usiku-hii ni dhana isiyo sahihi ambayo wengi wanayo:

<sup>28</sup>Farao akamwambia Musa,Nenda zako,uijangalie,usinione uso tena;kwani siku hiyo utakayoniangalia uso wangu utakufa.<sup>29</sup>Musa akasema,Umenena vema;mimi sitakuangalia uso tena.(Kutoka 10:28-29)

Baada ya kifo cha wazaliwa wa kwanza,Waisraeli walikuwa na wajibu wa kutekeleza kabla hawajaondoka Misri.Wangekaa ndani ya nyumba zao hadi asubuhi,na kulipopambazuka wangechoma mabakio ya kondoo ambaa hawakula,kuenda katika vijiji vya Wamisri mahali walipoishi na

kuwaomba fedha,dhahabu na nguo,kuyasanya na kuyafunga mali yo yote ambayo wangebeba pamoja na mifugo yao na kuanza safari ya miguu ya maili ishirini hadi Ramesesi ambapo walipanga safari ya kutoka Misri.Tazama:

<sup>34</sup>Watu wakauchukua unga wa mikate yao kabla haijatiwa chachu,na vyombo vyao vya kukandia wakavitia ndani ya nguo zao mabegani.<sup>35</sup>Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa;wakataka kwa Misri vyombo vya dhahabu,na mavazi.<sup>36</sup>BWANA akawajalia kupendelewa na Wamisri hata wakawapa kila walichokitaka.Nao wakawateka Wamisri nyara.<sup>37</sup>Wana wa Israeli wakasafiri kutoka Ramasesi mpaka Sukothi,walipata hesabu yao kama watu sita mia elfu watu waume waliokwenda kwa miguu,bila kuhesabu watoto.<sup>38</sup>Na kundi kubwa la watu waliochangamana mno wakakwea pamoja nao;na kondoo na ng'ombe,wanyama wengi sana.<sup>39</sup>Nao wakaoka mikate isiyochachwa ya ule unga waliouchukua walipopata Misri,maana,haukutiwa chachu,kwa sababu walitolewa watoke Misri,wasiweze kukawia,nao walikuwa hawajajifanya tayari chakula.(Kutoka 12:34-39)

Usiku wa Kungaliwa ndio usiku ambaao walitoka Ramasesi.Usiku ambaao walitoka Misri.

Baada ya kufanya walichoamuriwa na Mungu,walitoka.

Kutoka 13:18 inatuambia, "Kwa hiyo Mungu akawaongoza watu kuitia njia ya kuzunguka kuitia jangwani,kuelekea Bahari ya Shamu.Waisraeli walipanda kutoka katika nchi ya Misri wakiwa wamejiandaa kwa vita."

### **Mkate Usiotiwa Chachu**

Sisi Wakristo,twangundua kwamba Yesu alitulipia adhabu ya dhambi katika Pasaka na kwamba tunafaa tujaribu kuishi kama alivyoishi,bila dhambi na unafiki,ambapo chachu inaonyesha (Luka 12:1).

Hayati Herbert W.Armstrong aliandika kuhusu hili:

Na kama vile Waisraeli walitoka na mkono wenye nguvu (Hesabu 33:3),katika furaha na kushangilia juu ya ukombozi kutoka kwa utumwa,hivyo ndivyo Mkristo aliyekombolewa anaanza safari ya maisha ya Ukristo-juu katika mawingu ya furaha na shangwe.Lakini nini inafanyika?

Shetani na dhambi wanaanza kufuata mwana wa Mungu aliyekombolewa-na baadaye Mkristo aliyekombolewa karibu na hajawa na uzoefu anajipata chini kwenye kina cha kukatisha tamaa,na anajaribu kukata tamaa na kuacha safari.

Kumbuka Kutoka 14,kuanzia mstari wa 10-baada ya Waisraeli kuwaona jeshi kubwa likiwaifuata,walipoteza matumaini.Uwoga ukawaingilia.Wakaanza kunung'unika na kulalamika.Wakaona kwamba haingewezekana kuepuka Farao na jeshi lake,kwa sababu aliquwa na nguvu nyingi kuwashinda.Na wakawa wanyonge.Na hivyo ndivyo tulivyo.

### **Nguvu Zetu Hazitoshi!**

Lakini kumbuka ujumbe Mungu aliwapa kuitia kwa Musa: "Msio gope,simameni tu,mkauone wokovu wa BWANA

atakaowafanya leo;kwa maana hao  
Wamisri mliowaona leo hamtawaona  
tena milele.Bwana atawapigania ninyi”!  
Ni ajabu ilioje!

Hata tukiwa wanyonge,twaambia  
tusimame tu,na kuona wokovu wa  
Bwana.Atatupigania.Hatuwezi kushinda  
Shetani na dhambi,lakini Yeye  
anaweza.Yeye ndiye Mwokozi  
aliyefufuka-Kuhani wetu Mkuu-ambaye  
atusafisha-atatutakasa-na kutuokoa-  
na alisema hatatuacha!

Hatuwezi kutunza amri kwa nguvu zetu  
na mamlaka yetu.Lakini Kristo NDANI  
YETU anaweza kuzitunza! Lazima  
tumtegemee katika imani.(Armstrong  
HW.God's Holy Days-or Pagan Holidays-  
Which?-Worldwide Church of  
God,1976).

### **Madhumuni ya Sikukuu**

Lakini wacha tujifunze umuhimu wa  
Sikukuu.Kwa nini Mungu aliteuwa  
Sikukuu hizi? Ni nini ilikuwa  
MADHUMUNI yake kuu? Fungua Kutoka  
13,mstari wa 3: "...Musa akawaambia  
hao watu,Kumbukeni SIKU  
HII,MLIYOTOKA Misri..." Hii ilikuwa siku  
ya 15 ya Abibu.Mstari wa 6: "Mtakula  
mikate isiyochachwa muda wa siku saba  
itakuwa ni sikukuu ya BWANA  
Sikuukuu...Nafanya hivi kwa sababu ya  
jambo ambalo BWANA  
alinitendea[UKUMBUSHO] nilipotoka  
katika nchi ya Misri...na itakuwa  
"ISHARA"- (utambulisho wa THIBITISHO  
la kimiujiza)-"litakuwa kama alama  
kwenye mkono wako na UKUMBUSHO  
katika paji lako la uso"-KWA NINI?—"kwamba SHERIA YA BWANA INAPASWA

IWE KINYWANI MWAKO...Ni lazima  
UISHIKE amri hii..." (mistari ya 8,9 na  
10).

Haya,ndugu mpendwa,je,unaona  
maana yake ya kiajabu? Je!Unaelewa  
umuhimu wake? Je,unaona KUSUDI la  
Mungu? PASAKA inaonyesha KIFO CHA  
KRISTO kwa ondoleo la dhambi  
zilizopita.Kukubali damu yake haiwezi  
kumfanya mtu asamehewe dhambi  
alizotenda-haiwezi kukupa KIBALI cha  
kuendelea kutenda dhambi-kwa hivyo  
wakati tumekubali katika damu ya  
Yesu,dhambi zetu zinafutwa hadi wakati  
umefanya hivyo-Unasamehewa  
NDHAMBI ZILIZOPITA.

Lakini je,tutakomea hapo? Ya kwamba  
dhambi za kale zimesamehewa.Lakini  
bado sisi ni wanadamu wenye  
mwili.Bado tunapatwa na  
majaribu.Dhambi imetushika-  
tumekuwa WATUMWA wa dhambi,tuko  
chini ya nguvu zake.Na hatuna nguvu ya  
kujiokoa kutoka kwa dhambi!  
Tumekuwa katika KIFUNGO cha  
dhambi.Wacha tuelewe taswira-yaani  
maanake.(Amstrong HW.Kitu ambacho  
unapaswa kujua kuhusu Pasaka na  
Mikate Isiyotiwa Chachu.Good  
News,March 1979).

Kwa kiwango gani Wakristo wanapaswa  
kuondoa dhambi? Kama vile Yesu  
alivyofundisha, "mtakuwa mkamilifu,kama vile  
Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu"  
(Mathayo 5:48).Chachu inaonyesha aina ya  
dhambi (1 Wakorintho 5:7-8).Kama vile dhambi  
inavyofanya,chachu hufurisha.

Kama vile nambari saba inaonyesha  
ukamilifu,Wakristo wanafaa wafuate Pasaka na

siku saba za mikate isiyotiwa chachu. Maana na mfano wake haziwezi kukamilika na Pasaka peke yake. Pasaka inaonyesha kuikubali damu ya Kristo kama ondoleo la dhambi zilizopita na kifo cha Yesu.

Je,twaweza,kwa mfano,kumwacha Kristo akinin'inia kwenye mti aliyesulubiwa (Wagalatia 3:13)? Hapana.Siku saba ya Mikate isiyotiwa chachu zinazofuata Pasaka zinatusaidia kuonyesha kuondoa dhambi,kuzitunza amri kumi-baada ya dhambi zilizopita kusamehewa kwa sababu ya dhabihu ya Yesu.

Siku za Mikate Isiyotiwa chachu inaonyesha maisha na kazi ya Yesu aliyefufuka. Yesu alienda na kukaa kwenye kiti cha enzi cha Mungu ambapo anafanya kazi kwa bidii kwa niaba yetu kama Kuhani Mkuu,akitusafisha dhambi (Waebmania 2:17-18) akituokoa kabisa kutoka kwa nguvu za dhambi!

Haya ni yale yanayosemwa na maandiko ya Waebmania kuhusu Siku za Mikate Isiyotiwa Chachu:

<sup>15</sup>Mtakula mikate isiyochachwa muda wa siku saba;siku hiyo ya kwanza mtaondo chachu yote isiwe katika nyumba zenu kabisa;kwa kuwa mtu ye yote atakayekula mkate uliochachwa tangu siku hiyo ya kwanza hata siku ya saba,nafsi hiyo atakatiliwa mbali na Israeli.<sup>16</sup>Siku ya kwanza kutakuwa kwenu na kusanyiko takatifu;haitafanywa kazi yo yote katika siku hizo,isipokuwa kwa hiyo ambayo kila mtu hana budi kula,hiyo tu ifanyike kwenu.<sup>17</sup>Nanyi mtaitunza ile sikukuu ya mikate isiyochachwa;kwa kuwa katika siku iyo hiyo mimi nimeyatoa majeshi yenu katika nchi ya Misri;kwa hiyo

mtaitunza siku hiyo katika vizazi vyenu vyote,kwa amri ya milele.<sup>18</sup>Mwezi wa kwanza,siku ya kumi na nne wa mwezi,wakati wa jioni,mtakula mikate isiyochachwa,kuanzia jioni ya siku ya kumi na nne hadi jioni wa siku ya ishirini na moja.<sup>19</sup>Muda wa siku saba isionekane chachu katika nyumba zenu kabisa;kwa kuwa mtu ye yote atakayekula hiyo iliyotiwa chachu,nafsi hiyo atakatiliwa mbali na mukutano wa Israeli,akiwa mwenye kukaa hali ya ugeni,au akiwa mtu aliyezaliwa katika nchi.<sup>20</sup>Msile kitu chochote kilichochachwa;mtakula mikate isiyochachwa katika makao yenu yote (Kutoka 12:15-20)

Mambo ya Walawi 23:6-8 pia inafundisha hivyo.Na Kumbukumbu la Torati 16:16 inaonyesha kwamba matoleo yalikuwa yanatolewa katika Siku za Mikate Isiyotiwa Chachu,Pentekoste na katika Sikukuu za majira ya mapukutiko.

Awali,"sadaka za kuteketezwa na dhabihu" hazikuwepo "siku ile Mungu aliwatoa Misri"(Jeremia 7:22).Ziliongezwa kwa sababu ya kutotii (Jeremia 7:21-27) na Agano Jipya ni wazi kwamba hatuzihitaji sadaka za kuteketezwa ama dhabihu ya mnyama siku hizi (Waebmania 9:11-15).

Tunapokula mkate usiotiwa chachu kila siku hiyo ya sikukuu hiyo,twagundua kwamba tunapaswa kuepukana na dhambi ambazo zimekuwa nyingi katika ulimwengu unaotizingira.

### **Kufutiliwa Mbali au Kuadhimishwa?**

Je,Siku za Mikate Isiyotiwa Chachu zilifutiliwa mbali? Tazama kitu kingine ambacho Herbert W.Armstrong aliandika:

### **Haikuondolewa na Agano la Kale**

Kumbuka kwamba Siku za Mikate Isiyotiwa Chachu ni KIPINDI ambacho kina SABATO za kipekee.Na KIPINDI hiki kimesimamishwa MILELE-wakati Waisraeli bado walikuwa Misri kabla sheria ya maadhimisho ya Musa kupeanwa na kuandikwa-hata kabla Mungu hajaleta agano la kale! Kile ambacho hakikuletwa ama kusimamishwa,HAKIWEZI KUONDOLEWA! Katika tafsiri ya Fentoni,mstari wa 17 unatafsiriwa hivi: "Kwa hivyo Adhimisheni KIPINDI HIKI KAMA KIPINDI CHA MILELE." Kipindi chote kimejumuishwa.

Hili pekee lapaswa kuthibitisha kwamba SIKUKUU-na siku Saba za Mikate Isiyochachwa-zinadumu leo na hata MILELE!

Sasa kama mafungu haya yanahu tarehe 15,siyo tarehe 14,kama vile yanavyojulikana,na yamethibitishwa,basi je,Pasaka imeimarishwa MILELE? Ndiyo,imeimarishwa! Lakini mafungu haya yanahu SIKUKUU siyo PASAKA.Katika aya inayoanza Kutoka 12:21 PASAKA imetajwa na mstari wa 24 imeimarishwa MILELE!...

Kuadhimisha Pasaka peke yake,na kukosa kuadhimisha Sikuu ya Mikate Isiyochachwa kwa mfano inaonyesha

kumkubali damu ya Kristo na kuendelea kufanya dhambi-kusema SHERIA imefutiliwa,tuko chini ya neema,kumaanisha twaweza kuendelea kufanya dhambi!

Siku saba za Mikate Isiyochachwa zinaonyesha kutunza amri,ambayo ni njia nyingine ya kusema kuweka dhambi kando.(Armstrong HW.What You Should Know About the Passover and the Festival; of unleavened Bread.Good News,March 1979).

Wakristo wa awali hawakuamini ya kwamba Siku za Mikate Isiyochachwa zilifutiliwa mbali.Mtume Paulo aliunga mkono vilivyo kuadhimisha kwa siku hiyo na mkate usiyotiwa chachu (1 Wakorintho 5:7).Yeye na wengine bado walikuwa wakiadhimisha siku hizo na wakaifanya hivyo hata nje ya Yuda:

<sup>6</sup> Sisi tukatweka baada ya siku za mikate isiyotiwa chachu,tukatoka Filipi,tukawafikia Troa,safari ya siku tano,tukakaa huko siku saba.(Matendo 20:6)

Ikiwa Wakristo hawakuadhimisha Siku za Mikate Isiyochachwa,Roho Mtakatifu hangetia msukumo hayo yarekodiwe vile yalivyoandikwa.Basi Filipi ulikuwa mji wa kimataifa katika Makedonia.Ulikuwa ukitawaliwa na Warumi-kwa hivyo kuadhimisha siku hizi kulifanyika hata nje ya Yerusalem.Katika sehemu mbili za Agano Jipy,a tunaona kwamba Siku za Mikate Isiyochachwa ziliadhimishwa kwenye maeneo ya mataifa (1 Wakorintho 5:7;Matendo 20:6).

Kumbuka pia maelezo haya: "Siku hizo zilikuwa siku za mikate isiyochachwa" katika Matendo

12:3.Kwa vile Luka aliyejkuwa mwandishi wa kimataifa aliandikia Kitabu cha Matendo ya Mitume kwa mtaifa mwingine (Matendo 1:1),kwa nini alitaja siku hizi ikiwa hazikujulikana kwa Wakristo wa kimataifa na tena kama siku hizi hazikuwepo tena?

Pengine inafaa iongezwe kwamba mwongo wa karne ya tatu anayeitwa *Epistula Apostolarami* alidai kwamba Yesu na wanafunzi wake wanapaswa kuadhimisha siku za Mikate Isiyotiwa Chachu hadi Yesu arudi.Na kwa vile hatuwezi kutegemea hati hiyo,inaeleza kwamba wengine bado walikuwa wakiadhimisha siku hizo katika karne ya tatu.

Maeleo mengine yanayopatikana nje ya Biblia yanaripoti kwamba Mitume Paulo,Yohana na Filipo,na hata Polikapu wa Smirna na Wakristo wa awali,waliadhimisha siku za Mikate Isiyochachwa (Pionius.Life of Polycarp,Chapter2).

Licha ya hii,Kanuni 38 ya *baraza la Laodikia* ya karne ya nne(K.363-364) ilipiga marufuku kuadhimishwa kwa siku za Mikate isiyochachwa.Wengi katika Kanisa walikosa kuzingatia sheria ya baraza hilo ambayo ilienda kinyume cha Biblia na desturi ya Wakristo waaminifu wa awali.

Kwa hivyo Wasabato wengi waliendelea kuadhimisha Siku za Mikate Isiyochachwa baadaye(Pritz.Nazarene Jewish Christianity,Magnas,Jerusalem,1998,p.35;Jerome as cited in Pritz,pp.58,62,63;Ephipanius.The Panarion of Ephipanius of Salamis:Book II (sects 1-46) Section 1,Chapter 19,7-9.BRILL,1987,p.117-119) na hata Zama za Kati na mbeleni (Liechty D. Sabbatarianism in the Sixteenth Century.Andrews University

Press,Berrien Springs (MI),1993.pp.61-62;Falconer John.A Breife Refutation of John of John Traskes Judaical and Novel Fantyces,pp.57-58,as cited in the Ball B.Seventh Day Men:Sabbatarians and Sabbatarianism in England and Wales,1600-1800,2<sup>nd</sup> edition.James Clark & Co.,2009,pp.49-50).

Na sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea hatukubali kwamba Baraza la Laodikia liliongea kwa niaba ya Wakristo wa Kanisa la ukweli,na bado tunaadhimisha siku za Mikate Isiyochachwa.Tunakula mikate isiyochachwa kwa muda wa siku saba kama ilivyoamriwa kwa Biblia (Kutoka 12:15;13:6;23:15;34:18).Mikate huu unaweza kutengenezwa na nafaka tofauti-kutumia ngano tu siyo matarajio ya kibiblia.

(Pengine inafaa kutajwa kwamba mtu anaweza kula vyakula vingine tofauti na mkate usiochachwa wakati wa Sikukuu hii,ni kwamba mikate iliyochachwa ndiyo isiliwe.Pia,tofauti na Pasaka,siku ya kwanza na ya mwisho ya mikate Isiyochachwa ni kama Sabato ya kila wiki,ambazo mtu hatafanya kazi.)

Wakati wengine wanajaribu kuweka kama mafumbo sehemu nydingi za Biblia,hata hivyo kuna kuelewa kwa kiroho wa Sikukuu,pia kuna kuelewa wa kawaida.Na maadhimisho ya kawaida yanatusaidia kuelewa maana ya kiroho.

Siku za Mikate Isiyochachwa zinatusaidia kuelewa kwamba Wakristo wanapaswa kujitahidi kuepukana na dhambi na unafiki katika maisha yao (Mathayo 16:6-12;23:28;Luka 12:1).Kwa kuadhimisha siku hizi kimwili,twaweza kuelewa mafunzo ya kiroho ambayo Mungu anakusudia.

# JISOMEE KOZI YA

## BIBLIA

### JARIBIO LA 3 Masomo ya 9-12

Bob Thiel,Mhariri Mkuu

Utangulizi:Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na Kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka 1954,iliyoanza chini ya usimamizi wa hayati C.Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio.Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyo).Kadhalika imeongezwa vifungu toka Maandiko Matakatifu,pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali.

**Imechapishwa 2018 na Kanisa la Mungu Linaloendelea**

**Mtihani huu umepewa kukusaidia kuelewa Biblia yako vizuri.**

Basi sasa unasoma SEHEMU YA MASWALI.INABEBA MAAGIZO na MASWALI utakayoulizwa.Kumbuka kwamba kuna maswali 80 na kwamba yameorodheshwa yakifuatana 1,2,3 n.k.Pia kumbuka kwamba kuna majibu manne yanayopeanwa chini ya kilaswali.

Yameorodheshwa A,B,C and D.NI MOJA tu kati ya majibu manne haya ndilo jibu SAHIHI!-mengine matatu ni uwongo isipokuwa imetajwa.

UNAPASWA KUCHAGUA JIBU MOJA MIONGONI MWA MAJIBU MANNE.

Unapaswa kurudia utaratibu huo kwa kila swali.Huu ndio unahusu mtihani wako.(Kwa kawaida,majibu yasiyo sahihi ni dhana potofu ambazo zinafundishwa na kuaminwiwa kuhusu mada ya swali.)

Lengo letu ni kumpa ye yote anaye juhud la kumjua Mungu nafasi ya kuelewa maana kamili ya Biblia.

Kwa majibu unayotoa kwa maswali yetu,unasaidia kuonyesha ikiwa una haja ya kujifunza na unafanya bidii.Hakimu wa mwisho ambaye atahakikisha umejua Biblia yako na unaishi kwa kulingana na ukweli wa Biblia ni Mungu mwenyewe.Yeye ndiye awezaye kukupa uzima wa milele.

Hamu yako ya kusoma na kutengeneza nafasi yako ndiyo ya muhimu.Alama utakayopata si muhimu kwetu au kwako.Hata hivyo,kikawaida,twatarajia kwamba upate asilimia ya juu ya majibu sahihi kutoka kwako.

Jibu maswali mengi kulingana na uwezo wako bila kuangalia masomo yaliyopita.Ikiwa utapata swali gumu,basi uangalie masomo yaliyopita.Tunatarajia kwamba utafanya hivyo!

Kumbuka kwamba maswali haya yamegawanywa katika sehemu nne-kulingana na masomo manne.Tunakushauri kwamba usifanye zaidi ya somo moja kwa wakati mmoja.Chukua wakati ufaao kuelewa kila swali.

Yafuatayo ni MIFANO miwili YA KUKUONYESHA  
JINSI ya kuyajibu maswali:

Soma swalii la kwanza la jaribio hili.Jibu sahihi la kuchagua,hakika ni "C."Mfano wa pili ni huu:Tazama swalii la 2 kwenye ukurasa wa pili.Jibu sahihi ni "B." Hiyo ndiyo mifano vile ilivyo! Ni rahisi na upesi.

Utaratibu ni ule ule kila wakati.Basi endelea na swalii la 3 vilevile.

### **Mungu Anajidhahirisha!**

1.GANI kati ya maelezo manne haya ni ukweli?

- A.Tunapaswa kukubali-bila kuuliza swalii-neno la wahudumu wa kawaida kuhusu kuwepo kwa Mungu,ama kutowepo kwake.
- B.Mungu HAJATUAMURU kuhakikisha mambo yote.
- C.Mungu anatuamuru tuthibitishe kuwepo kwake.
- D.Hakuna njia yo yote unaweza kuthibitisha uwepo wa Mungu-unaweza kukubali tu mafundisho ya Biblia kwa imani.

2.GANI kati ya maelezo haya manne ni ukweli?

- A.Tuna wakati mwingi wa kuthibitisha kuwepo kwa Mungu-Adhabu yake ya ulimwengu huu ulioasi i katika nyakati zizazo.
- B.Mtu akihakikisha kwa haraka kwamba kuna Mungu basi anaishi vyema.
- C.Watu tayari wamejua Mungu hajakufa-kuwepo kwake milele si kitu cha kuthibitisha.
- D.Wale wanaopuruka kwenye sayari kutoka kwa "mazingira ya nje" wanaenda kuiteka sayari hii na kuitawala.

3.GANI kati ya maelezo haya manne ni UKWELI?

- A.Vifaa vyaa nguvu viko vyaa "kusikia" viumbe vyaa roho.
- B.Vifaa vyaa udadisi vyaa maabara ziko za 'kuona' viumbe vyaa roho.
- C.Binadamu ana uwezo wa "kuhisi" viumbe vyaa kiroho,na kuthibitisha kwamba viko.
- D.Wanadamu wanaweza KUJUA kwamba Mungu,ambaye- ni roho yupo kwa sababu anatimiza,kwa matukio halisi,unabii alisema kitambo.

4.Njia ya kusoma Biblia na Kozi hii ya Mawasiliano ni

- A.kusoma somo PEKEE-siyo Biblia.
- B.ni kuangalia maelezo ya Biblia tu bila kusumbuka na kuandika maandishi ama mafungu ya Biblia.
- C.kutoangalia Kamusi ya Biblia.
- D.kuangalia maelezo yote ya Biblia,na kusoma na kuandika hoja katika masomo mara kwa mara.

5.Enzi ya Mungu

- A.inapatikana katika mbingu ya pili.
- B.iko kwenye Mlima Zayuni kule Palestina leo.
- C.haipatikani kwenye Mlima wa Zayuni wa kiroho.
- D.ni hekalu la Yerusalemu wa mbinguni.

6.Ni gani kati ya yafuatayo yanaeleza Nyumba ya Daudi?

- A.Kibao cha Musa.
- B.Sanduku la James Osuari.
- C.Jiwe la Tel Dani.
- D.Hakuna,kwa vile hakuna uthibitisho.

- 7.GANI kati ya maelezo manne haya ni Kweli?
- A.Mungu hana AINA ya vitu vya dunia vinavyofananishwa na vya mbinguni.
  - B.Yerusalemu wa dunia ni AINA ya Yerusalemu wa mbinguni.
  - C.Mlima Zayuni wa mbinguni haungekuwa na mfano wa AINA ya mbinguni.
  - DMpango wa Mungu sio mara mbili.
- 8.Tuta: A.hatutaweza kuona vifaa vya kiroho.
- B.ona vifaa vya kiroho wakati "tutaenda mbinguni."
  - C.weza kuona vifaa vya kiroho wakati TUTAZALIWA na Mungu-tutakopabdalishwa kuwa viumbwe vya kiroho.
  - D.weza kuona vifaa vya kiroho ikiwa tutapatwa na moto wa Jehanamu.
- 9.Je Mungu,kwa kujieleza katika Ufunuo 1:13-16,anataka tuwe na ufahamu wa kumjua vile alivyo?
- A.Hapana-ingekuwa kosa kufanya hivyo.
  - B.Hakuna kusudi lo ote la kujua vile Mungu alivyo.
  - C.Ndiyo,ili awe halisi na binafsi sana kwetu.
  - D.Si vizuri tuamini kwamba anafanana hivyo vile ilivyoelezwa.
- 10.Wakati wanaoshinda wanatukuzwa,wata:
- A.wataonekana bila mwanga na wachofu.
  - B.ng'aa kama jua,lakini bila nguvu za kutosha.
  - C.ng'aa kama jua na kuwa na nguvu sana.
  - D.hawatakuwa tofauti na vile walivyo kwa wakati huu ambao wana mwili wa kufa.
- 11.Ni nani ana uwezo Mkubwa juu ya yote?
- A.Kristo,kwa sababu amefanya jukumu kubwa sana kuhusiana na binadamu.
  - B.Mungu Baba.
  - C.Hakuna mtu mkubwa-Baba na Kristo wote wana mamlaka sawa.
  - D.Baba na Kristo wanabadilishana kwa kuchukua nafasi ya mamlaka.
- 12.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni KWELI? Yesu Kristo:
- A.ndiye mara nyingi alijulikana kama BWANA/YHVH Mungu na mataifa ya Agano la Kale
  - B.alikuwa Neno,lakini siyo nembo.
  - C.alikuwa na mwanzo wa siku.
  - D.mara nyingi anaitwa Baba.
- 13.Moja kati ya washirika wawili wa Familia ya Mungu amejulikana kama BABA
- A.kwa sababu tumejua kwamba amekuwepo kabla ya nembo.
  - B.kwa sababu ya uhusiano kati yake na Yesu aliye Kristo.
  - C.kwa sababu imekuwa desturi ya madhehebu mengi kumwita "Baba yetu."
  - D.kwa sababu aliumba Nembo kabla hajauumba mbingu na nchi.
- 14.Je,Mungu amekuwepo milele?
- A.Kristo hajakuwepo katika umbo lo lote hadi Baba alipomzaa.
  - B.Hapana-Baba aligundua kwamba alikuwepo miaka mingi iliyopita.
  - C.Ni Baba pekee amekuwepo milele.
  - D.Ndiyo-Mungu ametuelezea kwenye Biblia.
- 15.GANI kati ya maelezo manne haya ni KWELI?
- A.Mtu Mtakatifu ambaye alikuja kuwa Yesu Kristo hakuwa "Msemaji" wa Familia ya Mungu katika nyakati za

Agano la Kale.  
B.Wakati Yesu atashinda ulimwengu wote,hatakuwa chini ya Baba  
C.Maneno "Hapo mwanzo..." (Mwanzo 1:1) hayaonyeshi wakati Familia ya Mungu waliumba Mbingu na Nchi.  
D.Biblia inafundisha uungu wa Baba na uungu wa Mwana.

16.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni KWELI?

- A.Baba na Mwana hawajawahi kuongelewa kama "Mungu."
- B.Kristo na Baba mara nyingi hawaelewani kuhusu vitu.
- C.Neno "BWANA" linaweza kumaanisha "Aliye na uhai nafsini mwake."
- D.Biblia inafundisha binafsi ya Roho Mtakatifu vile iliyofafanuliwa na wanaoamini utatu wa uungu.

17.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni KWELI?

- A.Hakuna awezaye kuyajua maarifa ya Mungu "yaliyofichika."
- B.Mawazo duni ya binadamu hayawesi kueleza maarifa makuu ya Mungu.
- C.Kuna kiwango cha kuelewa kwa Mungu.
- D.Wanadamu wanaweza kuzihesabu idadi ya nyota.

18.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni UKWELI?

- A.Mungu anajua mabilioni ya nyota na majina.
- B.Mungu hajui tabia ya kawaida ya watu.
- C.Mfumo wa Mawasiliano ya Mungu unafikia kiwango cha mwendo wa mwanga.
- D.Binadamu,kwa maarifa yao ya juu ya kisayansi na teknolojia ya

kisasa,watakuja kushinda ukuu wa Mungu.

19.Uzima wa milele unawezekana:

- A.Kupitia kwa "kizazi cha hapo kwa hapo."
- B.ikiwa umepeanwa kama zawadi ya bure na Mungu.
- C.Kupitia kwa mabadiliko ya kawaida ya mata.
- D.Kwa mchanganyiko wa gesi.

20.Je,Mungu anaweza kumpa mwanadamu nguvu yake?

- A.Hakuna rekodi ambayo imeonyesha kwamba Mungu anafanya hivyo.
- B.kuna rekodi ambazo zinaonyesha kwamba amewapa wengine nguvu isiyo ya kawaida ili wafanye miujiza.
- C.hakuna ahadi kwamba twaweza kuipokea nguvu za Roho Mtakatifu.
- D.hakuna rekodi yo yote inayoonyesha kwamba tunaweza kuipata nguvu hiyo.

21.Roho Mtakatifu:

- A.haina chochote kuhusu wazo la Mungu.
- B.haina nguvu sana leo hii.
- C.haswa ni nguvu na wazo la Mungu ambayo inaweza kuwa SEHEMU yako.
- D.inapatikana kwa ye yote wakati anapozaliwa.

22.Nguvu ya Roho wa Mungu

- A.haipatikani kila mahali.
- B.ni kitu ambacho kinaonekana.
- C.Haina kazi yo yote muhimu.
- D.ni nguvu ambayo inafanya mapenzi yake kila mahali duniani na mbinguni.

## **Unabii ni Thibitisho la Mungu!**

23.Sababu moja inayofanya wengine kukosa kuamini kwamba Mungu yupo:

- A.ni kwamba Mungu hajaacha uthibitisho wo wote wakuthibitisha kuwa yupo.
- B.mkosoaji ameogopa na anakosa kugundua uhakika ambao unabii wake unachukuliwa.
- C.Unabii wake umethibitishwa kwamba sio wa kutegemewa.
- D.wanakosa akili ya kuthibitisha kwamba Mungu yupo.

24.Unabii wa Mungu uliotimilika:

- A.umechukuliwa kwa kina sana.
- B.umechukuliwa kwa namna ya hafifu.
- C.umechukuliwa kwa njia duni sana.
- D.haujawai kuthibitisha uwepo wake.

25.Unabii unathibitisha zaidi ya kivuli cha shaka kwamba Mungu Yupo kwa sababu:

- A.hakuna binadamu ye yote ambaye angetabiri matukio na yafanyike halisi vile alivyofanya.
- B.thibitisho liko kwa Biblia na wengi wanaamini kwa Biblia.
- C.wahudumu wanasema hivyo.
- D.Somo hili lasema hivyo.

26.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni KWELI?

- A.ulimwengu unaamini kwamba unabii ni thibitisho la Mungu.
- B.manabii mara nyingi walitabiri kuhusu matukio yote ya Agano la Kale ambayo BAADAYE yalitimilika,na matukio ya siku zetu ambayo yanaendelea kutimizwa.
- C.watabiri na wataalamu wa uchumi wetu wanaweza kutabiri kama Mungu.
- D.wataalamu wa hewa wanaweza kutabiri kwa usahihi kama Mungu.

27.Watu wengi:

- A.wamesikia ukweli kila mahali kiasi kwamba wanaweza kukubali unabii wa Biblia bila kuuliza swali.
- B.wamesoma na kuthibitisha unabii wa Biblia na kuwepo kwa Mungu.
- C.hawajagundua kwamba kuwepo kwao kutategemea kuthibitisha kwa ukweli wa unabii wa Biblia na uwepo wa Mungu.
- D.wamejua Marekani katika unabii.

28.Je! Mungu anadai kwamba anaweza kusema kitu BILA KUKOSEA?

- A.Hapana-ana msukomsuko.
- B.Ndiyo-kwa sababu ana NGUVU ya kuutimiza unabii wote.
- C.Neno lake linasema anaweza.
- D.Anasita kufanya madai hayo.

29.Je,Mungu anasema kwamba wanadamu wana nguvu kama yake ya kuleta matukio kama alivyofanya.

- A.Ndiyo.
- B.Hapana.
- C.Hasemi chochote kwa njia moja au nydingine.
- D.Anasema kwamba wanadamu wanaweza kuititia kwa teknolojia.

30.Kosa KUBWA wasomi wengi wa ulimwengi huu wanafanya katika kutokubali Biblia kama Neno la ukweli la Mungu ni kwamba:

- A.WANAJIFANYA kwamba unabii wa Biblia sio sahihi ama hauna maana.
- B.wana nia sana ya kufanya mapenzi ya Mungu kuliko vile inavyotarajiwa.
- C.hawaamini wakosoaji.
- D.wanaamini katika Agano la Kale,lakini siyo kwa Agano Jipy.

31.Ni nini haswa husababisha matatizo mengi ya wanadamu?

A.uwezo wa mwanadamu kuleta amani.  
B.wanadamu kujipanga kwa kukandamiza maovu.  
C.tabia ya kuasi kwa mwanadamu.  
D.kukosa uwezo wa kuchagua daktari unaofaa.

32.GANI kat i ya maelezo haya yafuatayo ni KWELI?

A.Ukweli kwamba mwanadamu hajawahi kudumisha imani ya kudumu sio uthibitisho kwamba Neno la Mungu limetimizwa.  
B.Wanadamu hatimaye watadumisha amani ya ulimwengu bila kuingia kat i isiyo ya kawaida ya Mungu  
C.Mungu,ambaye anajua kiini cha matatizo ya binadamu,alitabiri kuanzia mwanzo kiwango cha huzuni ambayo dunia hii itapitia.  
D.Mungu hakujua kitambo mahali tabia ya uasi wa mwanadamu utampeleka.

33.Unabii wa Mungu wa ugomvi wa mwanadamu unaopita kwa vipindi vingi unathibitisha kuwepo kwake kwa sababu:

A.kadri watu wanavyozidi kuzuia,hawawezi.  
B.Kwa kujua udhaifu wao,wote wamegeukia Mungu ili wapate nguvu ya kubadilisha tabia zao.  
C.wakijua kwamba ni amri inayotoka kwa Mungu,wanaikubali kwa unyenyekevu kama ukweli.  
D.mara nyingi wanatambua kwamba huo ugomvi unaonyesha uwepo wa Mungu.

34.GANI kat i ya maelezo manne haya yafuatayo ni KWELI?

A.Unabii wa Mungu wa historia ya mbari ni uwongo.  
B.Ukoo wa Yafethi haujapanuliwa.  
C.Ukoo wa Hamu kila mara wamesimama juu ya wote.  
D.Mungu alitabiri kuhusu Mfalme Koreshi.

35.GANI kat i ya maelezo haya manne ni KWELI?

A.Mungu alitabiri sehemu muhimu za historia za ulimwengu mapema.  
B.Mungu mara nyingi hajatabiri vitu sahihi.  
C.Mungu bado atatabiri historia ya siku zijazo.  
D.Unabii ni mambo ya zamani.

36.Mungu anatuonyesha kwamba yupo leo:

A.kwa kuleta unabii mwangi wa nyakati za mwisho uliotabiriwa Karne nyingi utimike.  
B.kwa kutoruhusu falme kumi wa Muungano wa Ulaya kutokea.  
C.kuacha matukio ya uliwengu kujiunda peke yao.  
D.kuiondoa "mikono" yake katika masuala ya ulimengu huu.

37.Ugaidi:

A.ni jambo la kisasa tu.  
B.unaweza kusababishwa na ukoo wa Yafethi pekee.  
C.ulitabiriwa kuufanyika katika nyakati hizi za mwisho.  
D.hauwezi kuhusisha watu wa Mashariki ya Kati.

38.Yesu alifundisha kwamba kanisa la kweli:

A.watakuwa kundi dogo katika kipindi hiki.  
B.halitapata mateso.  
C.litatawala ulimwengu huu katika

nyakati hizi.

D.litakuwa na makao makuu huko Rumi  
kwa vipindi vyote vya kanisa.

39.Kanisa lililomwaminifu sana katika siku hizi  
za mwisho.

A.linaweka muundo utakaofuatwa na  
madhehebu mengi.

B.ni kubwa kwa ushirika.

C.ndilo pekee linatimiza maelezo ya lile  
alisema aatasababisha kuwepo (Ufunuo  
3:7-13) katika nyakati za mwisho.

D.linatangaza ujumbe ambao  
unapokelewa na kila mtu kwa furaha.

40.Baada ya Biblia kututhibitishia kwamba  
Mungu yupo,twafaa tufanye nini?

A.Sahau kila kitu.

B.Kumkubali kama Kiongozi wetu na  
kumfuata sheria zake ili tuishi uzima tele.

C.Tusibadilishe jinsi tunavyoishi.

D.Tusijali kuhusu yatakayokuja mbeleni.

41.GANI kati ya maelezo haya manne ni  
UKWELI?

A.Mageuzi ni ukweli uliothibitishwa,siyo  
nadharia.

B.Uumbaji sio ya kisayansi.

C.Mageuzi ni nadharia isiyo na  
thibitisho.

D.Uvumbuzi wa Sayansi mara nyingi  
hupinga Biblia.

42.Ikiwa utachukua Biblia vile ilivyo na kuiamini  
kwamba inasema vile imeandikwa,

A.utaamini kwamba mageuzi ni ukweli  
na hakuna "upande mwingine wa mageuzi."

B.unaonyesha kutojua kwako.

C.unaweza kuonyesha kejeli.

D.utachanganyikiwa na kupoteza  
wokovu wa milele.

43.GANI kati ya maelezo haya manne ni KWELI?

A.Ni Mungu pekee ndiye angeweza  
kuumba mata hapo mwanzo.

B.Mungu hakuwa na mpango wo wote  
wa kuweka mtindo wa dunia.

C.Mata imekuwepo kila mara.

D.Mungu hana nguvu ya kuumba kitu  
chochote.

44.Ni nini umuhimu wa madini ya URANI?

A.mionzo yake inathibitisha kwamba  
hakuna umilele wa mata.

B.Inaonyesha kwamba Mungu hayupo.

C.Haionyeshi cho chote.

D.Ni muhimu tu kwa vita vya atomiki.

45.Kwa vile mata imekuwepo kila mara.

A.hakuna maana ya kuwepo kwa  
Muumba.

B.mata ingejigeuka kutoka kwa kitu  
kisichokuwepo.

C.kuwepo kwake leo inahitaji Muumba.

D.hatuwezi kujuja kitu kuhusu mwanzo  
wa chochote.

46.Kuwepo kwa uhai:

A.kumeelezwa kinagaubaga na  
mageuzi.

B.kunaonyesha kwamba lazima Mungu  
awepo,kwa sababu uhai sio mali ya asili ya  
mata.

C.ni matokeo ya "kizazi hiari."

D.ni matokeo hasa ya "vitendo vya  
electroniki na kemia."

47.Kulingana na Nadharia ya Mageuzi,aina yote  
tofauti ya uhai:

A.lazima ungeumbwa na Mungu.

B.ulianza kutoka umati wa protoplazimu  
ya seli moja.

C.hauzai aina tofauti ya uhai mpya.

- D.Ni ya asili ya nguvu za ajabu,badala ya kawaida.
- 48.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni KWELI?
- A.Unaweza kuwa Mkristo wa ukweli na bado unaamini katika mageuzi kama mwanzo wa uhai.
  - B.Mageuzi ni thibitisho kwamba Biblia siyo ya Kisayansi.
  - C.Huwezi kuwa Mkristo wa ukweli na kuamini katika mageuzi kama mwanzo wa uhai.
  - D.Ujamaa kamwe hauwezi kupinga magaeuzi.
- 49.Ni nani kati ya hawa alithibitisha kwamba uhai unaweza kutoka kwa uhai pekee-ya kwamba hauwezi kutoka kwa hiari kutoka kwa mata iliyokufa.
- A.Aristola,mwanafalsafa Myunani.
  - B.Redi,Mtaliano.
  - C.Charles Darwin.
  - D.Kali Maksi.
- 50.Sheria ya "Biojenesisi" inasema kwamba:
- A.Biolojia ni thibitisho la mageuzi.
  - B.Kitabu cha Mwanzo sio ya kisayansi.
  - C.mata iliyokufa yenyewe inaweza kuleta uhai.
  - D.uhai unaweza kutokea tu kwa uhai.
- 51.Kulingana na Nadharia ya Mageuzi,
- A.mamalia wakaja kuwa wataambazi.
  - B.wanyama wa porini wasio na akili ni matokeo ya kuzorota.
  - C.mwanadamu alitoka kwa mpito wa polepole akawa mpya na tofauti na aina tata ya mnayama.
  - D.mwanadamu alichipuka kutoka kwa tumbili.
- 52.Aina mbali mbali ya uhai ambao unakaa juu ya dunia:
- A.ulitoka kwa mchakato wa mageuzi yasiyo na akili.
- B.inathibitisha kwamba aina ya uhai wa chini polepole ilikuja kuwa mpya na tofauti na baadaye ikawa aina tata ya uhai.
- C.inapinga maelezo ya uumbaji wa kitabu cha Mwanzo.
- D.kila mara inaishi ndani ya aina ya awali amba Mungu aliunda wakati wa uumbaji.
- 53.Kulingana na kitabu cha Mwanzo,
- A.Mungu aliumba mbingu na nchi.
  - B.aina tofauti ya uhai unaweza kuchipuka.
  - C.uhai wa mnyama ulikuwepo chini ya bahari mamilioni ya miaka kabla uhai wa miti kuanza kwenye ardhi.
  - D.uhai wote ulianza na mageuzi.
- 54.GANI kati ya maelezo haya manne ni UWONGO?
- A.Mabadiliko,kugeuka kwa ghafla ya asili,hayawesi kutengeneza AINA mpya.
  - B.aina mpya mbalimbali ni tofauti tu ndani ya aina ile ya MWANZO.
  - C.Aina mpya itatofautiana hadi zitakapokuja kuwa AINA MPYA.
  - D.Mabadiliko siyo thibitisho la Mageuzi.
- 55.Twaweza kuhitimisha kwamba:
- A.wanadamu mara nyingi wanapuuzia kimakusudi uthibitisho wa gharika.
  - B.hakuna miji ya kale iliyofuzikwa na gharika ya siku za Nuhu.
  - C.Visukuku vyote vilifunikwa baada ya muda wa mamilioni ya miaka.
  - D.visukuku vyepesi sana kila mara vilizikwa kwanza na vikubwa vikazikwa juu,basi ikathibitisha mageuzi kuwa ukweli.

56.GANI kati ya maelezo manne haya ni KWELI?

- A.aina nyepesi ya uhai mara nyingi huzikwa kwa utabakishaji wa chini.
- B.Aina tata ya uhai hautokei kwenye utabakishaji wa chini.
- C.Mageuzi yanathibitishwa na utaratibu wa kimantiki ambapo visukuku vinapatikana kama vimezikwa.
- D.Aina nyepesi na tata ya uhai mara nyingi hupatikana zikitawanyika kila mahali kwenye utabakishaji.

57.GANI kati ya maelezo manne yafuatayo ni UWONGO?

- A.Utabakishaji wa visukuku vya uharibifu kabla ya Adamu ziliwekwa kwenye mafuatano ya haraka kwa sababu mimea mara nyingi inapatikana ikipeleka mizizi kwa mafuatano ya matuta ya mawe!
- B.Matabaka yote yaliundwa tangia wakati wa Adamu,na yalifanya hivyo kwa sababu ya Gharika katika siku za Nuhu.
- C.Njia za wanyama wanaoruka angani,zilizohifadhiwa kwenye tabaka la kisukuku,zinathibitisha kwamba safu zinazofuatana ziliwekwa kwa kasi,kwa sababu nyayo zingefutika kabisa kwenye siku chache.
- D.Visikuku vingi vya nyakati kabla ya ulimwengu wa Adamu vilizikwa vikiwa hai na kwa ghafla.

58.Mungu AWALI aliumba dunia:

- A.Kamilifu na nzuri.
- B.Kwa vurugu na machafuko.
- C.kwa msongano moto unaoyeyuka ambayo haifai uhai.

D.imefunkwa na wingu na giza totoro.

59.Dunia IKAWA ukiwa kabla ya wakati wa Adamu:

- A.kwa sababu ya dhambi za watu walioishi kabla ya Adamu.
- B.kwa sababu ya dhambi za malaika ambao waliasi dhidi ya Mungu.
- C.kwa sababu Mungu hupenda kuharibu vitu.
- D.kwa sababu ya hali ya kawaida.

60.Katika mistari miwili ya kwanza ya Mwanzo,

- A.uumbaji kamilifu na uharibifu wake umefunuliwa.
- B.maelezo ya siku ya kwanza ya wiki ya uumbaji wa KIADAMU imerokodiwa.
- C.thibitisho limetolewa ambalo linaonyesha kwamba Mungu awali alizumba mbingu na nchi miaka 6,000 iliopita.
- D.tunapata kwamba dunia iliumbwaa katika machafuko.

61.Mageuzi yanaleta:

- A.angalau aina ya ukafiri.
- B.kuwa na imani thabiti katika Mungu.
- C.ufahamu wa kusudi la maisha.
- D.maarifa ya mwanzo wa vitu.

#### **HISTORIA NA AKIOLOJIA ZINATHIBITISHA KWAMBA BIBLIA NI UKWELI**

62.Biblia ni:

- A.udanganyifu wa wacha Mungu.
- B.jaribio la kwanza la wanadamu kujaribu kukusanya mapokeo ya kale na kufanya kwamba ni kazi ya Mungu.
- C.kitabu cha hekaya na hadithi.
- D.ufunuo uliotiwa msukumo kutoka kwa Mungu.

63.viongozi wa madhehebu ya ulimwengu wanaamini kwamba Biblia:

- A.inabeba hekaya na hadithi kuhusu Mungu,na sio ufunuo kutoka kwa Mungu kwa mwanadamu yenyе maarifa muhimu.
- B.inafaa wanadamu waitii kwa sababu Mungu aliyeitia msukumo ana mamlaka juu ya shughuli za wanadamu.
- C.ni ufunuo uliotiwa msukumo kutoka kwa Mungu ambayo ni maarifa mwafaka yanayohitajika na mwanadamu.
- D.ni neno lililotiwa msukumo na Mungu mwenyewe,na inafaa ifuatwe kwa kina sana.

64.Watu ambao hawaamini na hawafanyi kinachosemwa na Biblia

- A.bado wanaweza kuelewa maana ya matukio ya ulimwengu yanayofanyika kwa wakati huu.
- B.wanajua lengo la kuumbwa kwa binadamu na kuwekwa hapa duniani.
- C.hawawezi kuelewa masomo ya wakati uliopita,na hata pia hawawezi kujua kwa kina kitakachowapata watu katika wakati ujao.
- D.bado wanaweza kuamua peke yao kilicho kibaya na kilicho chema.

65.Uthibitisho wa kutiwa msukumo na uhakika wa Biblia

- A.haujakataliwa na wasomi wa ulimwengu.
- B.unaweza kupingwa na sayansi.
- C.umekanwa na ulimwengu kwa sababu ulimwengu unajua kwamba ikiwa Biblia imethibitishwa kuwa ya uhakika, watu wangeitii Biblia.
- D.unaweza kukataliwa kutoka kwa

rekodi sahihi ya kihistoria.

66.Katika Talmudi ya Wayahudi,ambayo ni rekodi ya kihistoria ya imani na matendo ya Wayahudi,Wayahudi walisema kwamba Yesu Kristo

- A.alifanya miujiza ya kuponya watu na kutoa mapepo.
- B.hakuwepo.
- C.alitenda miujiza kwa nguvu za Mungu.
- D.ndiye Masihi aliyetabiriwa katika Maandiko.

67.Mwanahistoria asiyekuwa Myahudi wa karne ya kwanza,Yusufu,alitamka kwamba

- A.Yesu ni hadithi tu iliyobuniwa na watu wa Mataifa.

- B.Yakobo alikuwa ndugu wa Yesu aliyeitwa Kristo.

- C.Yohana Mbatizaji alikuwa mtu mwovu.

- D.hakuna uthibitisho wowote wa kuunga mkono kuwa Yesu alikuwa na mwanafunzi ye yote.

68.Mamlaka na msukumo wa Biblia

- A.imekanwa bila kujaribiwa.
- B.imetambulika na wakalimani wote wa Biblia.
- C.imekuwa msingi wa desturi ya makanisa yote.
- D.imekanwa na wakafiri peke yake.

69.Watu wengi

- A.hawatilii maanani yanayosemwa na makanisa kuhusu Biblia.
- B.wanachunguza Biblia peke yao ili wapate kujua yananonenwa katika Biblia.
- C.kwa kawaida wanataka kuzuia tamaa zao na kufanya yanayonenwa na Biblia.
- D.hawataki kuamini hekaya kwa sababu

wanapenda ukweli.

70.GANI kati ya maelezo haya manne ni UWONGO?

- A.Watu mara nyingi wanakataa ukweli wa Biblia kama kitu kilichopitwa na wakati katika kipindi hiki cha kiteknolojia.
- B.Ni rahisi kwa watu waliolelewa katika makanisa tofauti kuelewa ukweli wa Biblia.
- C.Wanadamu kawaida wanadhani kwamba njia zao ni bora kuliko njia za Mungu.
- D.Vita,magonjwa na mateso ni adhabu ya njia potofu ya maisha.

71.Maelezo "Bwana akasema," ambayo yanapatikana mara mia katika Biblia,yanamaanisha kwamba

- A.Mungu anaongea nasi na mamlaka kupitia kwa Biblia.
- B.hatuhitaji kufanya yaliyonenwa na Mungu.
- C.manabii walioandika Biblia kimakosa walitoa dhana zao na kuziweka kama za Mungu.
- D.tunafaa tuamini kila kitu ambacho makanisa yanasema kuhusu Biblia.

72.Uhifadhi sahihi wa Biblia

- A.haujawahi kuthibitishwa.
- B.haijathibitishwa na hati ya Bahari Mfu.
- C.umeelezwa na Hati ya Isaya iliyopatikana mionganoni mwa Hati ya Bahari Mfu.
- D.hauna umuhimu halisi kwetu sisi leo hii.

73.GANI kati ya maelezo haya manne ni UWONGO?

- A.Kuna tofauti kidogo katika hati ya Waebrania na Wayunani ya Biblia.

B.Mungu aliruhusu mabadiliko machache ya kimaandishi katika matamshi na utaratibu wa maneno ili kwamba wale wanaoongea Kiebrania na Kiyunani watakuwa wakielewa Biblia hata kama lugha inabadilika polepole.

C.Mabadiliko machache hayabadilishi ujumbe muhimu wa Biblia.

D.Tofauti katika hati ya Kiebrania na Kiyunani ya Biblia ni ya kina sana kiasi kwamba maana ya Biblia imepotea.

74.Utafsiri mwingi wa Biblia

- A.unakinzana sana kiasi kwamba haiwezekani kuyajua aliyosema Mungu.
- B.ni wa maana kwa sababu lugha ya Kizungu inabadilika polepole baada ya karne yingi.
- C.haukusudiwa na Mungu.
- D.haungekuwepo kwa sababu Biblia haikusudiwa kusomwa na watu wa kawaida.

75.Toleo la Biblia ya Revised Standard Version

- A.ndiyo kamilifu.
- B.haipaswi kusomwa na mtu ye yote.
- C.ilitafsiriwa na wakomunisti kama mpango dhidi ya Ukristo.
- D.ni mbali sana na ukamilifu,lakini ni sahihi kiasi cha kutumiwa kama Neno la Mungu na Wakristo.

76.Je,tunayo Biblia yote?

- A.Ndiyo,ila tu vitabu visivyothibitishwa ambavyo vinafaa kuongezwa kwa Biblia.
- B.Hatuwezi kuwa na hakika kama tuko na Biblia yote.
- C.Hapani,hatuna Biblia yote.
- D.Ndiyo,tunayo;kwa sababu tunalo thibitisho kwamba Biblia imehifadhiwa kwa njia iliyosahihii.

77.Je,kunalo thibitisho kwamba Wazee wa Biblia waliwahi kuwepo?

A.Hakuna thibitisho.

B.Uthibitisho ni adimu sana na hauwezi kuwa na thamani yo yote.

C.Pengine,lakini thibitisho limepotea kabisa kwa karne nyingi.

D.Ndiyo kunalo,kwa sababu miji mingi katika Mesopotamia ilipewa majina baada ya majina yao!

78.Je,mataifa ya kale yalizingatia "Gharika ya Nuhu" kama ukweli wa Kihistoria?

A.Yote ilirekodi gharika ya Nuhu kama ukweli wa kihistoria.

B.Hawakuandika chochote kuhusu gharika hiyo.

C.Walikana kwamba haikutokezea Gharika hiyo.

D.Hatuwezi kujua kwa sababu rekodi zao zote zimepotea.

79.Je,kunao uthibitisho kwamba maelezo ya Biblia ya Yusufu kuwa katika Misri ni ukweli?

A.Hakuna uthibitisho ambao umekuwa wazi.

B.Hadithi ya Yusufu imethibitishwa kuwa hekaya ya Wayahudi.

C.Ushuhuda tele unathibitisha kwamba Yusufu alikuwa mtu wa kihistoria.

D.Haijalishi ikiwa kulikuwako na uthibitisho,kwa sababu Biblia ni kitabu kisichotegemewa kama VITABU VYA KAWAIDA vyta historia.

80.Je,wakoaji wako SAWA katika madi kwamba Kitabu cha Danieli ni ubunifu?

A.Hapana,hawako sawa.Hamna mstari wo wote wa Danieli ambao umethibitishwa kihistoria kuwa uwongo,Mistari mingi imethibitishwa kama ukweli.

B.Ndiyo,kwa sababu miujiza ambayo imerekodiwa kwa Kitabu hicho haingeweza kufanyika.

C.Hatuwezi kuwa na uhakika.  
D.Sehemu yake ni ubunifu na sehemu zake zingine ni ukweli kihistoria.  
Kwa vile Umemaliza.

### MAAGIZO YA MWISHO

Tunza sehemu hii ya maswali.Weka kwa daftari lako mwisho wa masomo haya yanayochambuliwa.Pitia maswali haya kila mara.Kwa nini? Kwa sababu mapitio hayo yatakupatia fursa ya kufurahia majibu ya kweli na kuyahifadhi akilini mwako.

Pia,mapitio ya majibu matatu yasiyo sahihi ambayo yamepeanwa katika kila swali yatakusaidia kugundua waziwazi baadhi ya dhana ambazo haujatilia maanani.Utashika na kutunza ukweli kwa njia iliyo bora sana ukiambia ukweli huo.

### MAJIBU YA JARIBIO LA 3:


1	1	1	2	3	4	5	64	73
-	0-	9-	8-	7-	6-	5-	-C	-D
C	C	B	B	C	B	A		
2	1	2	2	3	4	5	65	74
-	1-	0-	9-	8-	7-	6-	-C	-B
B	B	B	B	A	B	D		
3	1	2	3	3	4	5	66	75
-	2-	1-	0-	9-	8-	7-	-A	-D
D	A	C	A	C	C	B		
4	1	2	3	4	4	5	67	76
-	3-	2-	1-	0-	9-	8-	-B	-D
D	B	D	C	B	B	A		
5	1	2	3	4	5	5	68	77
-	4-	3-	2-	1-	0-	9-	-A	-D
D	D	B	C	C	D	B		
6	1	2	3	4	5	6	69	78
-	5-	4-	3-	2-	1-	0-	-A	-A
C	D	C	A	C	C	A		
7	1	2	3	4	5	6	70	79
-	6-	5-	4-	3-	2-	1-	-B	-C
B	C	A	D	A	D	A		
8	1	2	3	4	5	6	71	80
-	7-	6-	5-	4-	3-	2-	-A	-A
C	B	B	A	A	A	D		
9	1	2	3	4	5	6	72	
-	8-	7-	6-	5-	4-	3-	-C	
C	A	C	A	C	C	A		

Ujipe alama Mwenyewe:

Hesabu idadi ya maswali uliyokosea. Asilimia ya alama yako itakuwa karibu na nambari ifuatayo:

1-99	9-89	17-78
2-97	10-87	18-77
3-96	11-86	19-76
4-95	12-85	20-75
5-94	13-84	21-73
6-92	14-82	22-72
7-91	15-81	23-71
8-90	16-82	24-70

## Injili ya Ufalme na Lengo la Umoja wa Mataifa



Na Bob Thiel

### Je,Wanadamu Wana Suluhisho?

Ulimwengu unakabiliana na shida nyingi. Watu wengi wana njaa.Watu wengi wamekandamizwa.Watu wengi wanakabiliana na umaskini.Mataifa mengi yana madeni makubwa.Watoto pamoja na wale hawajazaliwa,wananyanyaswa.Magonjwa yanyoshinda madawa yanatatiza madaktari wengi.Miji mikubwa ina hewa iliyochafuliwa zaidi na haina afya.Wanasiasa wengi wanatishia vita.Mashambulizi ya kigaidi yanaendelea kutukia.

Je,viongozi wa ulimwengu wanaweza kutatua shida zinazokabili wanadamu?

Wengi wanadhani hivyo.

### Ajenda Mpya ya Ulimwengu

Mnamo Septemba 25,2015,baada ya hotuba muhimu ya Papa Francis wa Vatikani,mataifa 193 ya Umoja wa Mataifa (UM),walipiga kura kuyatekeleza "Malengo 17 ya Kudumu ya Maendeleo" ya awali yaliyopewa jina Ajenda

Mpya ya Ulimwengu.Haya ndiyo malengo 17 ya UM:

Lengo la 1.Kumaliza umaskini wa aina yo yote kila mahali.

Lengo la 2.Kumaliza njaa,kufikia usalama wa chakula na kuimarishe lishe bora na kukuza kilimo cha kudumu.

Lengo la 3.Kuhakikisha maisha bora na kuimarishe ustawi wo wote na kwa umma wote.

Lengo la 4.Kuhakikisha ujumla na shirika bora ya usawa na kuendeleza fursa ya elimu ya kudumu na nafasi kwa wote.

Lengo la 5.Kufanikisha usawa wa jinsia na kuwezesha wanawake na wasichana wote.

Lengo la 6.Kuhakikisha uwepo na usimamizi wa kudumu wa maji na usafi wa mazingira kwa wote.

Lengo la 7.Kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya kisasa kwa bei nafuu,ya kuaminika,ya kudumu kwa wote.

Lengo la 8.Kukuza,kujumuisha na kudumisha ukuaaji wa uchumi,ajira ya mafanikio na heshima kwa wote.

Lengo la 9.Kujenga miundombinu thabiti,kukuza ujenzi wa viwanda unaojumuisha za kudumu na kuendeleza uvumbuzi.

Lengo la 10.Kupunguza ukosefu wa usawa ndani ya mionganoni mwa nchi.

Lengo la 11.Kufanya miji na makazi ya wanadamu ya kujumuisha,imara na ya kudumu.

Lengo la 12.Kuhakikisha matumizi ya uzalishaji wa kudumu.

Lengo la 13.Kuchukua hatua ya dharura kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa na madhara yake.

Lengo la 14.Kuhifadhi na kudumisha matumizi ya bahari,maziwa na rasilimali ya bahari kwa maendeleo ya kudumu.

Lengo la 15.Kulinda,kurejesha na kuimarisha matumizi ya kudumu ya mazingira ya nchi kavu,usimamizi ya kudumu ya misitu,kupambana na majangwa na kusimamisha na kubadili uharibifu wa ardhi na kusimamisha kupotea kwa viumbhai.

Lengo 16.Kukuza amani na jamii za kujumuisha kwa kudumisha maendeleo,kutoa fursa ya haki kwa wote na kujenga ufanisi,ujaribaki na taasisi shirikishi katika ngazi zote.

Lengo la 17.Kuboresha njia za utekelezaji na kuumarisha ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo ya kudumu.

Ajenda hii inadhaniwa kutekelezwa kikamilifu ufikiapo mwaka wa 2030 na pia huitwa *Ajenda ya Maendeleo ya kudumu ya 2030*.Inalenga kusuluuhisha maradhi yanayokabiliana na wanadamu kuitia kwenye kanuni,elimu na ushirikiano wa kimataifa na madhehebu.Wakati shabaha zake ni nzuri,mbinu zake zingine na malengo yake ni mabaya (Mwanzo 3:4).Ajenda hii,pia ni sambamba na waraka wa Papa ya *Laudato si*.Papa Francis aliuita upitishaji wa *Ajenda Mpya ya Ulimwengi* "ishara muhimu ya matumaini."

Kwa kufutilia makubaliano ya UM,kulikuwako na mkutano kule Pari mnamo Desemba 2015 (kinachitwa kirasi *Mkutano wa Vyama kwa Mfumo wa Mkataba wa Mabadiliko ya hali ya Hewa*).Papa Francis pia alisifu makubaliano ya kimataifa na kuyashauri mataifa "kuyafuata kwa

makini njia iliyo mbele na akili inayokuwa kila wakati wa mshikamano."

Karibia mataifa yote katika ulimwengu walikubaliana na mkataba wa Pari ambao ulikuwa na dhamira haswa ya malengo ya kimazingira na kifedha.(Baadaye Rais wa Marekani Barack Obama aliatia sahihi hati ya kufanya Marekani wakubaliane na hayo mnamo mwaka wa 2016,lakini mnamo mwaka wa 2017,Rais wa Marekani Donald Trump alisema kwamba Marekani hawatakubaliana na mikataba ya Pari.Hii ilisababisha hasira ya kimataifa na ikasaidia kutenganisha Marekani na Ulaya na sehemu nyingi ya ulimwengu.)

Wakati hakuna anayetaka kupumua hewa iliyochafuka,kushinda njaa,kuwa maskini,kuwa katika hatari,n.k,je,mshikamano huu utasuluuhisha shida zinazokibili binadamu?

#### **Kufutilia Rekodi ya Muungano wa Mataifa**

Muungano wa Mataifa ulianzishwa na kuimarishwa mnamo tarehe 24 Oktoba,1945,baada ya vita vya ulimwengu wa II,iliuzuie mgogoro wa aina hiyo na kujaribu kukuza amani ulimwenguni.Wakati wa uanzilishi wake, muungano huu ulikuwa na mataifa 51,yako mataifa 193 sasa hivi.

Kumekuwako na migogoro zaidi ya mia,kama sivyo,maelfu ulimwenguni tangia Muungano wa Mataifa uundwe,lakini bado hatujakuwa na tunachokiita vita vya tatu vya ulimwengu.

Wengine wanaamini kwamba ushirikiano wa kimataifa kama Muungano wa kimataifa unaodaiwa kukuzwa ukiunganishwa na aina ya madhehebu na ajenda ya ekumeni ambayo Papa Francis na viongozi wengi wa dini wanajaribu kuimarisha,utaleta amani na ustawi.

Hata bivyo,kufuutilia rekodi ya Muungano wa Mataifa,kufanya hivi hakujakuwa vyema.Pamoja na migogoro mingi ya silaha tangia Muungano wa Mataifa uundwe,mamilioni wameishi njaa,wamekuwa wakimbizi,na/ama wamekuwa maskini hohe hahe.

Kwa muda wa mwongo mmoja uliopita,Muungano wa Mataifa ulipanga kuyatekeleza *Malengo ya Milenia*.Ulikuwa na "malengo manane ya maendeleo" lakini hii haikufua dafu,hata kulingana na Muungano wa Mataifa (MM) mwenyewe.Kwa hivyo,mnamo 2015,ulichoitwa "Malengo 17 ya kudumu ya maendeleo" yalipitishwa.Wengine wana matumaini.Wengine wanayachukua kama ndoto ya kubuni.

Kulingana na vile ndoto ya jamii timilifu inavyoenda,mnamo Mei 6,Papa Francis alisema kwamba aliota kuhusu jamii mema na timilifu ya Ulaya ambayo kanisa lake litasaidia bara hiyo kuifikisha.Lakini Biblia inasema kwamba ndoto hii ya Papa itabadilika kuwa ujinamizi (Ufunuo 18).

#### **Kutakuwako ma Ushirikiano Fulani na Mafanikio,Lakini...**

*Kamus ya Merriam Webster* inasema kwamba jamii timilifu ni "mahali panapodhaniwa kuwa kuna serikali,sheria na hali za kijamii timilifu."

Biblia inafundisha kwamba wanadaamu hawawezi kusuluhisha shida zao wenyewe:

23 Ee BWANA,najua kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake;kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu.(Yeremia 10:23)

Biblia inafundisha kwamba ushirikiano wa

kimataifa hautafaulu:

16 Uharibifu na mashaka yamo njiani mwao.17 Wala njia ya amani hawakuijua.18 Kumcha Mungu hakupo machoni pao (Warumi 3:16-18).

Ijapokuwa,wanadamu wengi wanajitahidi kuelekeza mtazamo wao wa jamii timilifu na hata wakati mwingine wanahuisha dini.Lakini hakuna anayetaka kufuata njia za Mungu mmoja wa Kweli.Siyo kwamba Muungano wa Mataifa ama malengo ya Vatikani.Kutakuwako na vikwazo vingine.

Kwa hakika,na pengine baada ya migogoro mikubwa,aina ya mkataba wa amani utakubaliwa na kuthibitishwa (Danieli 9:27).Baadaye wengi wataamini kimakosa kwamba wanadamu wataweza kuleta jamii ya amani na timilifu.

Wengi wataamini "mafanikio ya jamii timilifu" hiyo (Ezekieli 13:10) pamoja na ishara tofauti na miujiza (2 Wathesalonike 2:9-12).Lakini Biblia inasema amani kama hiyo haiwezi kudumu (Danieli 9:27;11:31-44),liche na kinachodaiwa na viongozi (Wathesalonike 5:3;Isaya 59:8).Dhana kwamba,bila Yesu Kristo,binadamu wanaweza kuleta jamii timilifu katika "dunia hii mbovu" ni injili potofu (Wagalatia 1:3-10).

Ikiwa wanadamu hawawezi kabisa kuleta jamii timilifu,je aina tofauti ya jamii timilifu itawezekana?

Ndiyo.

#### **Ni Injili Gani Yesu Alihubiri?**

Biblia inafundisha kwamba Jamii Timilifu inayoitwa Ufalme wa Mungu itachukua nafasi ya serikali za wanadamu (Danieli 2:44;Ufunuo 11:15;19:1-20).

Wakati Yesu alianza huduma yake ya umma, alianza na kuhubiri **injili ya Ufalme wa Mungu**. Yafuatayo ni ripoti ya Marko:

14 Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, Wakati umetimia, na Ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini Injili (Marko 1:14-15).

Neno injili, linatoka kwa neno la Ugiriki ambalo limetafsiriwa kama *euangelion*, na linamaanisha "ujumbe mzuri" ama "habari njema." Katika Agano Jipy, neno la Kiingereza la "Ufalme" ambalo linahusiana na ufalme wa Mungu, limetajwa karibia mara 149 katika Biblia ya Kiingereza ya NKJV na mara 151 katika Kiingereza ya *Douay Rheims*. Linatoka kwa neno la Kigiriki linalotafsiriwa kama *basileia* ambalo linaonyesha utawala ama milki ya wafalme.

Falme za wanadamu, kama vile Ufalme wa Mungu, una mfalme (Ufunuo 17:14), zinachukua eneo la kijiografia (Ufunuo 11:15), zina sheria (Isaya 2:3-4; 30:9), na zina watu wanaotawaliwa (Luka 13:29).

Yafuatayo ni mafundisho ya hadharani kutoka kwa Yesu ambayo Mathayo alirekodi:

23 Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme (Mathayo 4:23).

Mathayo pia anarekodi:

35 Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme (Mathayo 9:35).

Agano Jipy linaonyesha kwamba Yesu atatawala milele:

33 Atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho (Luka 1:33).

**Luka anarekodi kwamba kusudi lililomfanya Yesu kutumwa ni kuhubiri Ufalme wa Mungu.** Kumbuka alivyofundisha Yesu:

43 Akawaambia, imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa (Luka 4:43).

Je, umewah i kuisikia injili hii ikihubiriwa? Je, ushagundua kwamba kusudi kuu la Yesu alienda na kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu?

Luka pia anarekodi kwamba Yesu alienda na kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu:

10 Basi wale mitume waliporudi walimweleza mambo yote waliyoyatenda; akawachukua, akaenda nao faraghani mpaka mji mmoja uitwao Bethsaida. 11 Na makutano walipojua walimfuata; akawakaribisha, akawa akisema nao habari za ufalme wa Mungu (Luka 9:10-11).

Yesu alifundisha kwamba Ufalme wa Mungu unapaswa kuwa kipaumbele kwa wale amba watamfuata:

33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake (Mathayo 6:33).

31 Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. 32 Msio gope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme (Luka 12:31-32).

Wakristo wanafaa KUTAFUTA KWANZA Ufalme wa Mungu.Wanafanya hivi kwa kuiweka kama kipaumbele cha juu na kuishi kama Kristo angewahitaji waishi na kuangalia kurudi kwake na Ufalme wake.Na bado,wengi wanaokiri Kristo,siyo kwamba hawatafuti kwanza ufalme pekee lakini hawajui hata ufalme huo.Wengi pia wanaamini kimakosa kwamba kwa kushiriki siasa ya ulimwengu ndiyo Mungu anatarajia kutoka kwa Wakristo.Kwa kukosa kuelewa Ufalme wa Mungu,hawaishi sasa vile wanavyotakikana kuishi au hawaelewii kwa nini binadamu wamekuwa na dosari.

Kumbuka kwamba Ufalme utapewa kundi dogo (Warumi 11:5).Inahitaji unyenyekevu ili uwe sehemu ya kundi dogo la ukweli.

Hata kama wanadamu wanafikiri kwamba ni werevu sana,kuna upungufu katika kuelewa kwetu,lakini Mungu "akili zake hazina mpaka" (Zaburi 147:5).

Ndiyo maana Mungu ataingia kati ili aokoe sayari hii.

Wakati wengi wanaamini Mungu,watu wengi hawako tayari kuishi jinsi anavyoagiza.Tazama yafuatayo:

<sup>8</sup> Ee mwanadamu,yeye amekuonyesha yaliyo mema;na BWANA anataka nini kwako,ili kutenda haki,na kupenda rehema,na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! (Mika 6:8)

Kutembea kwa unyenyekevu na Mungu siyo kitu wanadamu wanataka kufanya.Kuanzia wakati wa Adamu na Hawa (Mwanzo 3:1-6),wanadamu wameamua kujitegemea mawazo yao na vipaumbele vyao bila kutanguliza Mungu,liche ya amri zake (Kutoka 20:3-17).

Kitabu cha Mithali kinafundisha:

<sup>5</sup> Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote,Wala usitegemee akili zako mwenyewe.<sup>6</sup> Katika njia zako zote mkiri yeye,Naye atayanyosha mapito yako.<sup>7</sup>Usiwe mwenye hekima machoni pak'o;Mche BWANA,ukajiepushe na uovu.(Mithali 3:5-7)

Na bado wengi hawatategemea Mungu na mioyo yao yote ama wamngojee yeye awaongoze.Wengi wanasema kwamba watafanya yanayotakikana na Mungu,lakini mwishowe hawafanyi.Wanadamu wamedanganywa na Shetani (Ufunuo 12:9) na wameangukia tamaa za ulimwengu na "kiburi cha uzima" (1 Yohana 2:16).

Kwa hivyo,wengi wamekuja na mapokeo yao ya kidini na serikali isiyo ya Mungu,kwa sababu wanadhani kwamba wanajua zaidi.Hata hivyo hawajui chochote (Yeremia 10:23) na hata wengi hawatatubu vilivyo.

Hiyo ndiyo maana wanadamu wanahitaji Ufalme wa Mungu (Mathayo 24:21-22).

### Njia za Mungu ni Sawa

Ukweli ni kwamba Mungu ni upendo (1 Yohana 4:8,16) na Mungu SIO mbinafsi.Amri za Mungu zinaonyesha upendo kwa Mungu na kwa majirani (Marko 12:29-31;Yakobo 2:8-11).Njia za ulimwengu ni za kibinafsni na zinaongoza kwa mauti (Warumi 8:6).

Kumbuka kwamba Biblia inaonyesha kwamba Wakristo halisi walitunza amri:

<sup>1</sup>Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu.Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa,ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye.<sup>2</sup> Katika

hii twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu,tumpendapo Mungu,na kuzishika amri zake.<sup>3</sup> Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu,kwamba tuzishike amri zake;wala amri zake si nzito.(1 Yohana 5:1-3)

"Amri zote za Mungu ni haki" (Zaburi 119:172).Njia zake ni safi (1 Timotheo 1:15).Kwa huzuni,wengi wamekubali aina tofauti ya "uasi" na hawatambui kwamba Yesu hakuja kuharibu amri ama manabii,lakini alikuja kuwakamilisha (Mathayo 5:17).Yesu alifundisha kwamba "mtu atakayezitenda na kuzifundisha,huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 5:19) (neno Ufalme wa Mungu na Ufalme wa Mbinguni linafanana).

Biblia inafundisha kwamba imani bila matendo imekufa (Yakobo 2:17).Wengi wanadai kwamba wanamfuata Yesu lakini hawataamini hakika mafundisho yake (Mathayo 7:21-23) na hawatamuiga kama vile inavyotakikana (1 Wakorintho 11:1). "Dhambi ni uasi wa amri." (1 Yohana 3:4,KJV) na wote wametenda dhambi (Warumi 3:23).Hata hivyo Biblia inaonyesha kwamba neema inashinda juu ya hukumu (Yakobo 2:13) kwa vile Mungu ana mpango na watu wote (Luka 3:6).

Suluhisho la wanadamu,tofauti na njia za Mungu,halitafanya kazi.Katika ufalme wa miaka elfu,Yesu "atatawala kwa fimbo ya chuma" (Ufunuo 19:15),na wema utaongoza kwa sababu watu wataishi kwa njia za Mungu.**Shida ZOTE za ulimwengu zinakuwepo kwa sababu jamii ya ulimwengu huu wamekataa kumtii Mungu na amri zake.** Historia inaonyesha kwamba binadnamu hawezi kusuluhiha shida za jamii:

<sup>6</sup> Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti;bali nia ya roho ni uzima na amani.<sup>7</sup> Kwa

kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu,kwa maana haitii sheria ya Mungu,wala haiwezi kuitii.<sup>8</sup> Wale wafuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.(Warumi 8:6-8)

Wakristo wanapaswa kuzingatia mambo ya kiroho,na wamepewa Roho Mtakatifu siku hizi (Warumi 8:9),liche ya udhaifu wetu:

<sup>26</sup> Maana,ndugu zangu,angalieni mwito wenu,ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini,si wengi wenye nguvu,si wengi wenye cheo walioitwa;  
<sup>27</sup> bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaabishe wenye hekima;tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaabishe vyenye nguvu;<sup>28</sup> tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa,naam,vitu ambavyo haviko,ili avibatilishe vile vilivyoko;<sup>29</sup> mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu.<sup>30</sup> Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu,aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu,na haki,na utakatifu,na ukombozi;<sup>31</sup> kusudi,kama ilivyoandikwa,Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.(1 Wakorintho 1:26-31)

Wakristo wanafaa kumtukuza Mungu katika mpango wake! Tunatembea kwa imani sasa (2 Wakorintho 5:7),tukitazama yaliyo juu (Wakolosai 3:2) katika imani (Waebrania 11:6).Tutabarikiwa kwa kutunza amri za Mungu (Ufunuo 22:14).Biblia inasema kwamba Wakristo watatawala na Yesu,lakini je,unagundua kwamba Wakristo halisi watatawala juu ya miji? Yesu alifundisha:

<sup>12</sup> Basi akasema,Mtu mmoja kabaila,alisafiri kwenda nchi ya mbali,ili ajipatie Ufalme na kurudi.<sup>13</sup> Akaita watu kumi katika watumwa wake,akawapa mafungu kumi ya fedha,akawaambia,Fanyeni biashara hata nitakapokuja.<sup>14</sup> Lakini watu wa mji wake walimchukia,wakatuma wajumbe kumfuata na kusema,Hatumtaki huyu atutawale.<sup>15</sup> Ikawa aliporudi ameupata ufalme wake,aliamuru waitwe wale watumwa aliowapa fedha,ili ajue faida aliyopata kila mtu kwa biashara yake.<sup>16</sup> Akaja wa kwanza,akasema,Bwana fungu lako limeleta faida ya mafungu kumi zaidi.<sup>17</sup> Akamwambia,vema,mtu mwemba;kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo,uwe na mamlaka juu ya miji kumi.<sup>18</sup> Akaja wa pili,akasema,Bwana,fungu lako limeleta matano faida.<sup>19</sup> Akamwambia huyu naye,Wewe uwe juu ya miji mitano.(Luka 19:12-19)

Uwe mwaminifu kwa madogo uliyo nayo sasa.Wakristo watapata fursa ya kutawala miji halisi,katika ufalme halisi.Yesu pia alisema, "ujira wangu u pamoja nami,kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo 22:12).Mungu ana mpango (Ayubu 14:15) na mahali (Yohana 14:2) kwa wale ambao watakubali kusikia wito wake (Yohana 6:44;Ufunuo 17:14).Ufalme wa Mungu ni halisi na unaweza kuwa sehemu yake!

Mwanzo wa 2016,jarida la *Sayansi* lilikuwa na makala lenye mada "Nguvu ya umati" ambayo ilisema kwamba akili ya kibandia na kupokea ujumbe kutoka kwa umati zinaweza kusuluhisha "shida za uovu" ambazo zinakumba binadamu.Hata hivyo,makala hii haikuelewa maana ya uovu,wacha hata kuusuluhisha uovu.

Ushirikiano,bila kuzifuata njia kweli za Mungu,hautafaulu katika karne ya 21 kama ilivyokuwa hapo nyuma baada ya Gharika Kuu wakati wanadamu walishirikiana kujenga Mnara wa Babeli (Mwanzo 11:1-9).

Shida za ulimwengu,haswa Mashariki ya Kati (liche ya faida ambazo hazitadumu,k.v.Danieli 9:27a,1 Wathesalonike 5:3),hazitasuluhishwa na wanadamu-twahitaji amani ya Ufalme wa Mungu (Warumi 14:17).

Shida za ugaidi wa kimataifa,liche ya faida inayotarajiwa,hautasuluhishwa (Ezekiel 21:12) na Umoja wa Mataifa ambao wamedanganywa (Ufunuo 12:9)-twahitaji furaha na faraja ya Ufalme wa Mungu.

Shida za mazingira hautasuluhishwa na ushirikiano wa kimataifa,kwa sababu mataifa ya ulimwengu watasaidia kuharibu dunia (Ufunuo 11:18),lakini zitasuluhishwa na Ufalme wa Mungu.

Shida za usinzi,utoaji mimba na kuuza sehemu za mwili wa mwanadamu na Marekani hazitasuluhishwa na mwanadamu lakini Ufalme wa Mungu.

Deni kubwa ambazo Marekani,Uingereza na mataifa mengi wanazo hazitasuluhishwa kuititia kwa wakala wa kimataifa,lakini mwishowe (baada ya uharibifu kulingana na Habakuki 2:6-8) na Ufalme wa Mungu.Ujinga na kukosa elimu hazitasuluhishwa na Umoja wa Mataifa-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Ugomvi wa dinihautasuluhishwa na harakati ya muungano wa madhehebu unaokubaliana na wokovu bila Yesu wa ukweli wa Biblia.Dhambi ndiyo SHIDA katika ulimwengu na kwa hivyo,twahitaji kutolewa sadaka kwa Yesu na kurudi kwake katika Ufalme wa Mungu.

Maswala ya njaa hayatasuluhishwa na mazao yenyе vinasaba ambayo yanaweka ulimwengu katika hatari ya njaa kwa sababu ya mimea kutofaulu-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Sayansi ya matibabu ya kisasa haina majawabu yote ya afya ya wanadamu-twahitaji Ufalme wa Mungu.Umaskini kubwa katika sehemu za Afrika,Asia na sehemu zingine,wakati watafaulu kidogo kwa muda kutoka kwa Babeli wa siku za mwisho (Ufunuo 18:1-19),hazitasuluhisha shida za umaskini-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Awamu ya miaka elfu ya Ufalme wa Mungu ni ufalme halisi ambaو utasimamishwa duniani.Utajengwa juu ya sheria ya Mungu na Mungu mwenye upendo kama kiongozi.Watakatifu watatawala na Kristo kwa miaka elfu (Ufunuo 5:10;20:4-6).Huu Ufalme utakuwa na watu ambaو kwa ukweli wako katika Kanisa la Mungu,lakini hakuna maandiko yanayoeleza ya kwamba Kanisa ni Ufalme (Ya Kikatoliki ama maandiko mengine).Kanisa la Rumi wamepinga mafundisho ya ufalme wa miaka elfu,na baadaye litapinga kwa nguvu ujumbe wa injili ya Biblia tukikaribia kufika mwisho.Na hii itavuta sana vyombo vya habari ambayo itasaidia kutimiza Mathayo 24:14.

Katika awamu yake ya mwisho,ufalme wa Mungu utajumuisha "Yerusalemu mpya,ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu" (Ufunuo 21:2) na katika maongeo yake hayatakuwa na mwisho.Hakutakuwepo na udhalimu tena na huzuni na mauti tena.

Kuhubiri na kuelewa injili ya Ufalme wa Mungu ni mada muhimu sana ya Biblia.Waandishi wa Agano la Kale waliifundisha njili hiyo.Yesu,Paulo na Yohana waliifundisha injili hiyo.

Mahubiri ya kale yaliyo nje ya Agano Jipy (ambayo yanaitwa Klementi wa 2) yalifundisha ufalme.Viongozi wa awali wa karne za kwanza kama Polycarp na Melito,waliifundisha injili hii.Sisi katika Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG) tunafundisha injili hii leo.

Ufalme wa Mungu ndio mada ya kwanza Yesu alihubiri (Marko 1:15).Hiyo ndio injili alihubiri mara baada ya kufufuka (Matendo 1:3)-na ni kitu Wakristo wanapaswa kuutafuta kwanza.

Injili haihusu maisha na kifo pekee ya Yesu.Msisitizo wa injili ambaو Yesu na wanafunzi wake walifundisha ulikuwa ni Ufalme wa Mungu unaokuja.Injili ya Ufalme inabeba wokovu kupitia kwa Kristo,na pia inahu mafundisho ya mwisho wa serikali za wanadamu (Ufunuo 11:15).

Kumbuka Yesu alifundisha kwamba mwisho hautafika mpaka injili ya Ufalme wa Mungu uhubiriwe ulimwenguni kama ushuhuda kwa mataifa yote (Mathayo 24:14).Na mahubiri yanaendelea sasa.

Habari njema ni kwamba **Ufalme wa Mungu ndio suluhisho la shida zinazokabili wanadamu**.Ijapokuwa wengi hawataki kukubali,kusikia na hata kuamini ukweli wake.Ufalme wa Mungu ni wa milele (Mathayo 6:13),wakati "ulimwengu huu unapita" (1 Wakorintho 7:31).

Kutangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu ndiko tunafanya kwa bidii katika Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG).Tunajitahidi kufundisha mambo yote ambayo Biblia inafundisha (Mathayo 28:19-20),pamoja na Ufalme wa Mungu (Mathayo 24:14).Wakati tunaungoja Ufalme,twahitaji kujifunza na kuzifuata njia za Mungu na kufariji wengine ambaو wanataka kuamini ukweli.Je,utaunga mkono kutangaza kwa ajili ya kurudi kwa Ufalme wa Mungu? Je,utaamini injili ya Ufalme wa Mungu?

KUITEKELEZA MATHAYO 24:14  
PAMOJA NA  
MATHAYO 28:19-20

KANISA LA MUNGU LINALOENDELEA  
[WWW.CCOG.ORG](http://WWW.CCOG.ORG)  
TAARIFA ZA UNABII WA BIBLIA ZA KILASIKU  
[WWW.COGRITER.COM](http://WWW.COGRITER.COM)



CCOG.ASIA:HII NI TOVUTI ILENGAYO WASOMAJI KUTOKA ASIA.INAZO MAKALA KATIKA LUGHA YA KICHINA CHA MANDARIN PIA NA KATIKA KIINGEREZA PAMOJA NA LUGHA ZINGINE ZA KIASIA.

CCOG.EU:HII NI TOVUTI KWA WALE WA ULAYA.INAZO MAKALA KATIKA LUGHA NYINGI ZA ULAYA.

CCOG.IN:HII NI TOVUTI INAYOLENGA WALIO WA ASILI YA KIHINDI.

CCOG.NZ:HII NI TOVUTI INAYOLENGA WALIO WA ASILI YA NEW ZEALAND.

CCOGCANADA.CA:HII NI TOVUTI INAYOLENGA WALIO WA ASILI YA CANADA.

CDLIDD.ES:HII NI KANISA LA MUNGU LINALOENDELEA (CCOG) KATIKA LUGHA YA KIHISPANIA.

PNHIND.PH:HII NI TOVUTI KWA AJILI YA WALE WA UFLIPINO AMA WENYE ASILI YAO.



Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia  
[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](http://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)  
Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)  
[www.youtube.com/continuingcog](http://www.youtube.com/continuingcog)

KANISA LA MUNGU LINALOENDELEA (CCOG) PIA HUTUMIA MAJARIDA PAMOJA NA MAGAZETI YA KIELEKTRONIKI,VITAVU NA BARUA ZA KILA JUMA KWA WAUMINI WAKE KUTEKELEZA  
MATHAYO 24:14 PAMOJA NA MATHAYO 28:19-20.

Swahili edition

